# TANGA YETU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MKUU WA MKOA TANGA**

## KARIBU TANGA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN



* Umetupatia Bilioni 429.1 kuboresha bandari
* Umeimarisha sekta ya afya
* Matumizi ya TEHAMA yanachochea fursa kwa vijana







**FEBRUARI, 2025**

# KARIBU TANGA RAIS SAMIA, T



**Mkuu wa Mkoa wa Tanga
Mhe Balozi Batilda S. Burian**

Karibu mpendwa msomaji wa Jarida hili la Tanga Yetu lililo mahususi , linalochapishwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, kama moja ya nyenzo inayotumika kuueleza umma, kwa taarifa sahihi na zinazowasilishwa kwa weledi kuhusu uhalisia wa maendeleo na ustawi wa wakazi wa mkoa huu.

Ni fahari kubwa sana kwetu wana-Tanga kwamba Jarida hili linatoka wakati ambapo Mhe Dk Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anafanya ziara ya kikazi mkoani kwetu.

Hivyo, sina budi kwanza kumshuruku Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma, kwa kutujalia uhai na afya njema, lakini zaidi kwa kumkirimia mema mengi, nguvu nyingi, hekima na busara, Mhe Rais Dk Samia, na hivyo kuendelea kutuongoza vema Watanzania.

Pili nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe Rais Dk Samia, kwa kutujali, kututhamini na kupanga muda wake kuja kukaa nasi wakazi waTanga ambapo atafika maeneo ya mkoa huu kuongea uso kwa uso na Watanzania wenzake.

Ni fursa adhimu na ya nadra sana kutokea, si hapa nchini pekee, lakini hata kwa mataifa mengine. Kupata wasaa wa kukutana na Mhe Rais wa nchi si jambo jepesi. Na hii inachangiwa na majukumu makubwa waliyonayo kwa Taifa.

Ziara yake kwetu Tanga ni ishara ya wazi ya namna Mhe Rais Dk Samia alivyojaliwa upendo wa kupindukia kwa wananchi wake. Wana-Tanga tunasema kwa kauli moja, asante sana Mama mpendwa, Mhe Rais Dk Samia.

Tunatambua. Upendo wakohuu ni deni kubwa sana kwetu. Usiwe na shaka. Wakati ukifika na ulio muafaka, unaofaa mwaka huu inshallah, tutakulipa deni hili kwa njia za kidemokrasia na kishindo kikubwa.

Ndugu zangu, tukirejea kwenye Jarida hili, ni jambo lililo dhahiri kwamba Tanga ni miongoni mwa mikoa 31 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Unapohitaji kubaini kasi ya maendeleo katika nyanja tofauti za kisekta kwa kipindi cha utawala wa takribani miaka minne ya Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan, itahitaji nafasi kubwa ya kuandika, na muda mrefu zaidi kuyaelezea kwa ufasaha mafanikio yaliyopatikana.

Mathalani, thamani ya miradi inayotekelezwa kwa fedha zilizotolewa na Serikali ya Mhe Dk Samia mkoani Tanga, ni jumla ya Shilingi 3.1 ikihusisha sekta za elimu, afya, maji, barabara, nishati, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), uwezeshaji wananchi kiuchumi, biashara na uwekezaji, miradi ya wafadhili, kilimo, mifugo, uvuvi, TASAF, Utawala, TEMESA na ardhi.

Ni kutokana hali hiyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeamua kuchapisha Jarida hili lenye kuwasilisha sehemu tu ya maendeleo na ustawi wa wakazi wa Tanga katika sekta kama vile elimu, miundombinu, afya, utawala bora, ugatuaji wa madaraka, maliasili, kilimo, uchumi wa buluu, utalii na mengine mengi yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika mkoani humu.

Mfano mdogo unaotoa taswira pana ya kiasi hicho cha fedha na mafanikio yake kwa jamii ni katika elimu, ambapo kwa mwaka 2024/2024 pekee, Mhe Rais Dk Samia ametupatia Shilingi bilioni 21.079 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za msingi 1,026.

Hatua hiyo ni ongezeko la madarasa 550 ikilinganishwa na 476 yaliyojengwa katika mwaka 2022/2023.

Aidha, kwa upande wa shule za sekondari kwa kipindi hicho, Tanga ilipokea Shilingi bilioni 25.673 kwa ujenzi wa madarasa 1,225, ikiwa ni ongezeko la madarasa 927 ikilinganishwa na madarasa 298 yaliyojengwa 2022/2023.

Ukiacha madarasa, fedha nyingine nyingi zilitolewa kwa ujenzi wa nyumba za walimu, mabweni, matundu ya vyoo, ujenzi wa shule mpya ikiwemo Shule ya wasichana Tanga

***Inaendelea uk 3***

# TUNAJIVUNIAUONGOZIWAKO



Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan

*Inatoka uk 2*

iliyopo Mabalanga wilayani Kilindi na utekelezaji wa mpango wa elimu ya msingi bila malipo.

Ndani ya Jarida hili, zipo taarifa na picha mbalimbali zinazoonesha ukweli wa miradi, huduma na fursa zilizopo mkoani Tanga.

Tumetoa umuhimu wa pekee kuweka tafsiri ya matokeo chanya ya matumizi ya fedha zilizotolewa na Mhe Rais Dk Samia kwenye miradi na huduma husika.

Ndio maana, unapotaja ukubwa wa miradi iliyopata fedha kutoka kwa Mhe Rais Dk Samia, hautosita kuitaja bandari la Tanga iliyopokea kiasi cha Shilingi bilioni 429.1 na kuleta mabadiliko yenye tija, ambayo hayakuwahi kutokea mkoani humu.

Ikumbukwe kwamba bandari hii ni kongwe iliyoanzishwa mwaka 1880 na wakoloni wa Kijerumani, na gati ya kwanza ilijengwa 1914, ikiwa na urefu wa mita 221. Gati ya pili ilijengwa 1954 ikiwa na urefu wa mita 229.

Uwekezaji wa maboresho uliofanyika umeongeza viwangoå katika utendaji kazi, kupungua kwa muda wa kuhudumia meli kutoka siku tano hadi mbili, huku TPA ikihudumia tani 1, 191,480 sawa na asilimia 93.4 ya tani 1,276,800 kwa kipindi cha 2023/2024.

Ni dhahiri kwamba uendelezaji wa miundombinu ya bandari hiyo, utazidi kuchochea ukuaji wa mapato, na hivyo kuchagiza kasi ya utoaji huduma unaofanywa na Serikali kwa wananchi wake.

Kama nilivyoeleza awali, yaliyomo kwenye Jarida ni sehemu tu iliyowekwa kama ishara ya kuonesha maendeleo makubwa ambayo mkoa wa Tanga ‘inapiga’ kupitia uongozi wa Mhe Rais Dk Samia, na sisi wasaidizi wake katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuyasimamia kwa uadilifu wote.

Ninachukua fursa hii kukukaribisha msomaji wetu na wote wenye mapenzi mema, kuwa na utulivu wa kutosha kulisoma Jarida hili ambalo mbali na kuelezea ukubwa wamiradi ya maendeleo, lakini linawasilisha, japo kwa uchache, fursa mbalimbali zinazopatikana mkoani Tanga na ambazo unaweza kuwa mnufaika wake.

Zipo fursa katika sekta za madini, kilimo, ufugaji, viwanda, elimu na utalii ukiwemo wa mali kale, nakadhalika.

Unapowekeza mkoani Tanga, ipo mianya thabiti ya kuvusha mazao na huduma zinazozalishwa kwenda maeneo mengine ya nchi, kwa vile mkoa huu unaunganishwa vizuri na mikoa mingine kwa njia za barabara, anga na majini.

Lakini pia Tanga inaunganishwa na masoko ya mataifa ya jirani hususani katika ukanda wa Afrika Mashariki, na ndio maana kwa ujumla wake tunasema, **Tanga Lango Kuu la Uchumi Afrika Mashariki.**

Mungu ibariki Afrika,
Mungu ibariki Tanzania.

# NIDHAMU NA UTII VINAVYOSHAMIRISHA

WAKATI huu, wakazi wa Tanga wanapoendelea kushirikishana mafanikio na kasi kubwa ya maendeleo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dk Samia Suluhu Hassan, atakuwa mkoani Tanga kwa ziara ya kikazi.

Ni faraja kubwa kwa wakazi wa Tanga, kwa namna mbili kubwa. Moja, ni kuendelea kupata huduma na ujenzi wa miundombinu bora ya kisekta kwa maendeleo na ustawi wao; pili, mtoaji wa fedha zinazofanikisha mafanikio hayo, yaani Mhe Rais Dk Samia, atakuwepo mkoani Tanga.

Hivyo, ni ishara ya wazi kwamba, umma unaposhuhudia kasi kubwa ya maendeleo na ustawi wa watu nchini, mkoa wa Tanga unawekwa kwenye orodha ya wanufaika wa mafanikio hayo.

Nyanja hizo ni pamoja miradi ya maendeleo inayojumuisha ujenzi wa miundombinu, afya, ubunifu, uanzishaji,



Katibu Tawala Mkoa wa Tanga Pili Mnyema

uendelezaji na usimamizi wa miradi na ukusanyaji wa mapato yanayochangia utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa jamii.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Sekretarieti ya Mkoa ninayoingoza, imekuwa kiungo muhimu kati ya wizara za kisekta, asasi za kiraia, sekta binafsi na mamlaka za serikali za mitaa, kuwezesha mazingira mazuri ya ushirikishwaji wa umma, unaochochea azma ya kujiletea maendeleo.

Katika uboreshaji wa utoaji huduma unaojali matakwa ya wananchi, na kwa kutambua ukubwa na kasi ya maendeleo, vinavyoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Sekretarieti ya Mkoa inayatambua na kuyahudumiwa kwa haki na usawa makundi yote ya jamii, na kwa kuzingatia zaidi Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Serikali.

Miongoni mwa uwajibikaji huo ni katika usimamizi wa utekelezaji wa maagizo na miradi ya Serikali, na ile inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo, tukitambua kwamba kila jambo linalofanyika kwa maslahi mapana ya umma, linawahusu wananchi tunaowahudumia.

Usimamizi bora wa miradi unafanyika kupitia Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara na Vitengo vya Sekretarieti ya Mkoa

Hayo yote yanafanyika kwa kufuata na kutekeleza maagizo na maelekezo ya Mhe Mkuu wa Mkoa wetu, Mhe Balozi Dk Batilda

Ndio maana, tunapochapisha Jarida hili ambalo wito wangu kwenu ni kulisoma kwa makini, na kutoa maoni

# ...HUDUMA BORA KWA WATUMISHI TANGA

kupitia njia za mawasiliano zilizotajwa ndani, ama ama kufika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuonana na uongozi, tunawajibika kupokea pongezi, kukosolewa ama kusahihishwa kadri ya maono na uelewa wa msomaji wetu tunayekujali na kukuthamini kwa kiwango kikubwa sana.

Ni kwa mukhtadha huo, Sekretarieti ya Mkoa inayapokea hayo yote kwa misingi ya haki na usawa, na kutoa mrejesho kadri ya kila jambo lilivyowasilishwa.

Ndugu wasomaji wa Jarida hili, Sekretarieti ya Mkoa inatekeleza majukumu yake yakiwemo kuhakikisha umma unapata taarifa sahihi na za kweli kuhusiana na masuala mbalimbali yanayowahusu, ikiwemo miradi ya maendeleo na huduma za jamii zinazowagusa kwenye maeneo ya mkoa wetu wa Tanga.

Na moja ya njia za uwailishaji taarifa kwa umma ni kupitia vyombo vya habari likiwemo Jarida hili, ama mitandao yetu ya kijamii na vyombo vingine visivyokuwa vya Serikali ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa washirika wetu wa karibu sana katika tasnia ya habari na mawasiliano.

Karibuni tuendelee kulisoma Jarida hili, ili kupata habari mbalimbali zinazohusu mkoa wetu na Tanga, lakini kuzibaini fursa mbalimbali zinazofungamana na shughuli za uzalishaji na ufikishaji mazao ama bidhaa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi, ikiwemo ukanda wa Afrika Mashariki.

Ndio maana tunasisitiza kwa kusema, **Tanga, Lango Kuu la Uchumi Afrika Mashariki.**



*Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (wa tatu kushoto) akiwa na Maafisa Mawasiliano wa Sekretarieti ya Mkoa, Afisa Habari wa Jiji na Mamlaka ya Maji (TangaUWASA) ambao taasisi zao zilitunukiwa vyeti vya utumishi bora kwenye tasnia hizo na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo hivi karibuni.*

# IJUE TANGA NA HIST



*Uwanja wa mpira wa Mkwakwani ni miongoni mwa miundombinu inayopendezesha mandhari ya jiji la Tanga.*

**Na Laban Mussa, OMM TANGA**

TANGA ni miongoni mwa maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi, yenye sifa lukuki ikiwemo ukarimu wa wakazi wakazi. Ikawa sababu y ahata sasa kuwepo wa msemo usemao, *Tanga waja leo, kuondoka ni majaaliwa.*

Yapo masimulizi tofauti yanayouelezea mkoa wa Tanga, miongoni mwake ni kumbukumbu za awali zilizoandikwa na kuhifadhiwa na Wareno.

Kumbukumbu hizo zinabainisha kuwa Tanga ni mahali ambapo kituo cha biashara kilichoanzishwa na Wareno ikiwa, ni sehemu ya utawala wao katika pwani ya Afrika Mashariki na waliudhibiti mji huo kwa zaidi ya miaka 200, yaani kati ya mwaka 1500 and 1700.

Wareno wanatajwa kuwepo kwenye Tanga hadi Sultani wa Oman alipopigana vita dhidi yao (Wareno), akawashinda na kuchukua utawala wa Tanga katikati ya mwaka 1700.

Ushindi huo ulimuwezesha Mreno kuyatwaa na maeneo ya jirani ya Mombasa, kisiwa cha Pemba na mji wa Kilwa Kisiwani mkoani Lindi.

Baada ya kuwashinda Wareno, Tanga iliendelea kubaki kuwa bandari ya biashara ya pembe za ndovu na watumwa chini ya utawala wa Sultani.

Pia, mji wa Tanga ukaendelea kuwa kitovu bora cha biashara ya watumwa kwa Waarabu hadi mwaka 1873 ambapo biashara hiyo ilipigwa marufuku.

Mwaka 1891 ikiwa ni katika karne ya 19, kulikuwa na kasi ya kukua kwa mataifa ya Ulaya kuligombea bara la Afrika, hivyo kuliwafanya Wajerumani kuja Tanga.

Wajerumani walinunua eneo la ukingo wa pwani katika Tanzania Bara (Tanganyika) kutoka kwa Sultani.

Hatua ya Wajerumani kutwaa maeneo hayo kuliifanya Tanga kuwa mji wa kwanza wa utawala wa Ujerumani katika Afrika Mashariki. Tanga ikawa Makao Makuu ya utawala wa kikoloni wa Wajerumani kabla ya kupelekwa Dar es Salaam mwanzoni mwa karne ya 20.

Pia, Tanga ilichaguliwa kuwa kituo cha kwanza cha kijeshi cha utawala wa Wajerumani katika Afrika Mashariki mwaka 1889, na kuwa ofisi ya wilaya ya kwanza mwaka 1891.

Mji huu ulishuhudia kasi ya ukuaji na mpangilio wake wakati wa utawala wa Wajerumani.

Katika historia hiyo, reli ya kwanza ilijengwa kwenye maeneo ya barabara kwa ajili ya usafiri na usafirishaji wa ndani ya mjini Tanga; na bandari ya kwanza kwa kusafirisha mazao ya kilimo hasa mkonge na kahawa kwenda nje ya nchi.

Mwaka 1896, ujenzi wa reli ya kwanza ya Usambara ulianza na uliendelea hadi mjini Moshi ilipofika mwaka 1912.

Tangu awali, uchumi wa Tanga

# TORIA ISIYOFUTIKA

ulitokana zaidi na kilimo cha mkonge, kilichotegemewa na wakoloni miaka kadhaa iliyopita.

Tukio jingine linalokumbukwa katika hostoria ya Tanga ni kwamba wakati huo, idadi ya watu iliongezeka kwa kasi kutokana na kuanzishwa kwa bandari ya kwanza mjini humo.

Shule ya Sekondari ya Old Tanga ilijengwa na utawala wa Kijerumani miaka ya 1890, ikiwa ni shule rasmi ya kwanza ya sekondari inayomilikiwa na serikali nchini Tanzania.

Pia, hospitali ya Bombo (sasa ni hospitali ya rufaa) ilijengwa na Wajerumani mwaka 1901, ikiwa ni hospitali ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mnamo tarehe 25 Agosti, 1919, jeshi la polisi lililojulikana kama Tanganyika Police Force lilianzishwa na mkoloni wa Kiingereza na ikatangazwa kwa tamko la Serikali ya Uingereza Na. 21-2583. Makao Makuu yake yalikuwa wilayani Lushoto, ingawa mwaka 1930 yalihamishiwa kwenda jijini Dar es Salaam.

Ikulu ya pili katika ukanda wa Afrika Mashariki ilijengwa wilayani Lushoto mwaka 1952 na utawala wa Kijerumani.

Mwaka 1922, chama cha watumishi wa umma kilichojulikana kama *Tanganyika Territory African Civil ServicesAssociation,* kiliundwa na Tanga kuwa Makao Makuu yake.

Wakati wa Uhuru, Tanga ulikuwa mji wa pili kwa ukubwa baada ya Dar es Salaam. Mji wa Tanga upo kwenye eneo la kimkakati kijiografia, takribani kilomita 100 hadi kufika bandari ya Mombasa nchini Kenya, kilomita 350 kwenda Mlima Kilimanjaro ulio mrefu kuliko milima yote barani Afrika, kilomita 360 kutoka bandari ya Dar es Salaam.

Kwa upande wa usafiri wa anga, inachukua muda wa nusu saa kusafiri kwa ndege kutoka Tanga hadi visiwani Zanzibar; hali inayotoa mazingira bora ya kiuchumi na kijamii kwa wafanyabiashara na watoa huduma wanaowekeza Tanga.



*Jengo la kitega uchumi lililopo Kange jijini Tanga.*

# LUSHOTO YAJA NA UTALII WA BARIDI




*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian, akiwa kwenye kilele cha Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Maganga wilayani Lushoto.*

**Na Mashaka Mgeta, OMM TANGA**

Pamoja na mandhari iliyoghubikwa na vilima vyenye miti ya asili, viumbe wa kupendeza kama ndege na vipepeo, na hewa nzuri, wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, imeibua utalii wa baridi, ambao haukuwepo kwenye orodha zake kama sehemu ya kivutio cha utalii.

Utalii huo unawekewa mzizi wake kwenye Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Magamba unaosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Hifadhi hiyo ina ukubwa wa hekta 9283.9 na imezungukwa na vijiji 21 vyenye jumla ya wakazi 57,347.

Programu za kuwezesha uhifadhi wa msitu huu zinafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi na Idadi ya Watu (UNDP), GEF na wadau mbalimbali.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa TFS - Kanda ya Kaskazini, James Nshare aliyasema hayo hivi karibuni, alipokuwa akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian.

Mhe Balozi Dk Batilda, alipanda hadi mwinuko wa mita 91 kufika kilele cha Kigulu Hakwewa kilichopo mita 1,840 kutoka usawa wa habari.

Mhe Balozi Dk Batilda na ujumbe wake, ulitembelea Pango la Mjerumani lililojengwa wakati wa ukoloni, lenye urefu wa mita 50, likiwa umbali wa mita 131 kutoka kilele cha Kigulu Hakwewa, kisha akatembea mita 191 kufika eneo la awali, na kufanya mzungukoa wa jumla ya mita 413.

Nshare alisema uanzishwaji wa utalii wa baridi unaendelea vema, na kwamba ongezeko la wawekezaji katika huduma za chakula na malazi, linaboresha mazingira kwa watalii.

Alisema TFS utalii mwingine unaoanzishwa ni kupanda kwenye kileleni kwa kutumia chombo kinachoendeshwa kwenye waya maalum ambayo awali, ilitumika kusafirishia magogo, ekolojia, nyama choma na michezo ikiwemo uendeshaji farasi.

Mhe Balozi Dk Batilda ameipongea TFS kwa hatua hiyo yenye kutekeleza maono ya Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan, kwamba TFS iondokane kutegemea kuni na mbao, badala yake ibuni miradi mbadala ya kutumia misitu kuingiza mapato.



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian akitoka kwenye handaki la Mjerumani lililopo msitu wa Magamba.*

# TANGA 'YAZIKIMBILIA' TANI 10,000 UZALISHAJI KOROSHO

Na Mwandishi Wetu, CBT

Serikali kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025 imeweka lengo la kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi kitaifa kufikia tani 700,000 ifikapo 2026.

Mbinu za kupata ongezeko la uzalishaji huo ni kuimarisha huduma za ugani, wakulima kufuata na kutumia mbinu na kanuni za kilimo bora cha korosho, usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa ruzuku ya asilimia mia moja kwa wakulima, usimamizi wa mauzo ya korosho ghafi kupitia mfumo wa stakabadhi mazao ghalani na kuratibu ubanguaji.

Tanga ni moja ya mikoa ya asili inayolima korosho, ikitanguliwa na Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani. Kwa sasa, kuna ongezeko la 'mikoa mipya' kwa kilimo cha korosho ikiwemo Singida, Dodoma, Tabora, Songwe, Iringa, Njombe, Katavi, Kilimanjaro, Kigoma, Morogoro na Mbeya.

**Uendelezaji korosho Tanga**

CBT kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, imeweka malengo ili kufikia uzalishaji wa tani 10,000 ifikapo 2025/2026.

Aidha, ili kufikia lengo hilo, mikakati iliyowekwa ni pamoja na :-

**Kuimarisha huduma ugani**

Kati ya 2022 hadi sasa, kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, CBT imeratibu mafunzo ya kilimo bora cha korosho kwa wakulima 5,459 kwenye halmashauri za wilaya zinazolima zao hilo.

Msimu wa 2024/2025, CBT imetekeleza mpango wa Jengo Kesho Iliyobora (BBT) Internship Offer kwa Maafisa Ugani Kilimo 500 nchini, kwa mkataba wa mwaka mmoja kutoka katika mpango wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT) uliopo Wizara ya Kilimo.

Kati ya vijana hao Mkoa wa Tanga umepata vijana 24 katika halmashauri za Mkinga (6), Pangani (6), Handeni (6), Korogwe (4) na Handeni Mji (2).



*Uoteshaji wa mbegu bora za korosho*

**Mbegu bora za korosho**

CBT imesambaza mbegu/miche bora ya korosho kwa wakulima kupitia Mamlaka za Serikali za Wilaya. Katika msimu wa 2023/2024, Mkoa ulisambaziwa kilogramu 5,994 za mbegu bora ya korosho zenye thamani ya takribani Shilingi milioni 22 na 2024/2025 ukapokea kilogramu 10,910 zenye thamani ya Shilingi milioni 54.7.

Nyingine ni uimarishaji wa masoko ya korosho, ukusanyaji na uuzwaji wa korosho unaoendelea mkoani Tanga.



*Vijana wanaoshiriki mpango wa Boresha Kesho Iliyobora (BBT) wakishiriki mafunzo kwa vitendo masuala ya udhibiti ubora kwenye kilimo cha korosho, Duga jijini Tanga.*

# BILIONI 429 ZA UBORESHAJI BANDARI Z



*Meli zikiwa zimetia nanga kwenye bandari ya Tanga.*

**Na Mashaka Mgeta, OMM TANGA**

BANDARI ya Tanga ni miongoni mwa bandari kuu tatu zilizopo mwambao mwa bahari ya Hindi, zinazosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Bandari hiyo inajumuisha pia bandari ndogo nne za Pangani, Kipumbwi, Mkwaja na Sahare, zinazohudumia shehena na abiria katika ukanda wa kaskazini mwa nchi na mwambao wa bahari.

Bandari hiyo yenye eneo la ukubwa wa hekta 17, inamiliki maeneo mengine mawili mkoani humo, moja ni Chongoleani lililopo kilomita 28 kutoka bandarini lenye ukubwa wa hekta 207 ambapo hekta 75 kati ya hizo, zinatumika kwa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Eneo jingine lipo Mwambani, kilometa sita kutoka bandarini lenye hekta 174 na linatumika kwa uwekezaji wa bandari kavu.

Meneja wa TPA mkoa wa Tanga, Masoud Mrisha anasema mwaka 2019, Serikali ilichukua hatua madhubuti za uboreshaji wa bandari hiyo kongwe, ili kukabiliana na changamoto zilizokuwepo na hivyo kuongheza ubora wa huduma na mapato.

Anasema changamoto zilizokuwepo, zilichangiwa kwa kiasi kikubwa na miundombinu duni na ukosefu wa vifaa vya kisasa katika utendaji kazi wa bandari.

Vyanzo mbalimbali vinaeleza kuwa bandari ya Tanga ilianzishwa 1880 na wakoloni wa Kijerumani, ambapo gati ya kwanza yenye mita 221 ilijengwa 1914, na gati la pili lenye mita 229 ikajengwa 1954.

Gati hizo zikawa na urefu wa jumla ya mita 450, wakati kina cha maji kilikuwa mita tatu na uwezo wa kuhudumia shehena tani 750,000 kwa mwaka.

Miundombinu hiyo ikaifanya bandari ya Tanga kutokuwa na uwezo wa kupokea meli gatini, badala yake, upakiaji na upakuaji mizigo ukafanyikia baharini, umbali wa kilometa 1.7 kutoka gatini, mahali meli zilipotia nanga.

## Uboreshaji wa bandari

Ili kukabiliana na hali hiyo,Serikali ikaboresha miundombinu ya bandari kupitia mradi wa kimkakati wa maboresho ya kwa awamu mbili zilizogharimu Shilingi Shilingi bilioni 429.1.

***Inaendelea uk 11***

# ZILIVYOCHECHEMUA UCHUMI WA TANGA

*Inatoka uk 10*

Katika awamu ya kwanza ya maboresho, TPA ilisaini mkataba na Mkandarasi, kampuni ya M/S China Habour Engineering Company (CHEC) Agosti 3, 2019 na ujenzi ulianza rasmi Oktoba 2019, ukakamilika Juni 2022. Awamu hiyo iligharimu Shilingi bilioni 172.3.

Oktoba 24, 2019, TPA ilisaini mkataba mwingine na kampuni za M/s NIRAS A/S (AS A LEAD Firm) ya Denmark kwa ushirikiano na M/S Maritime & Transport Business Solution, M/S ILF Consulting Engineers na M/S Anova Consult Company Limited ya Tanzania kwa ajili ya upembuzi yakinifu, kusimamia mikataba ya ujenzi wa gati na kuongeza kina cha bandari hiyo.

Utekelezaji wa mradi huo ulihusisha upanuzi wa eneo la kuingia na kutoka bandarini lenye upana wa mita 135, uchimbaji wa kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13, upanuzi wa eneo la kugeuzia meli kuwa na kipenyo cha mita 800 na ununuzi wa mitambo 16 ya kuhudumia shehena.

Ununuzi wa mitambo ya kuhudumia shehena ulihusisha mashine mbili za kupakia na kupakua mizigo, inayojulikana kama Diesel Electrical Operated Mobile Habour Ccrane yenye uzito wa tani 100, Forklift moja yenye uzito wa tani 16, Forklift moja ya uzito wa tani tano, Bale Clamp mbili zenye tani tatu, Front Loader moja ya tani 50, Empty Container Handler yenye tani 16, Terminal Tractor mbili, Grab yenye tani 15, Rubber Tyred Gantry (RTG) yenye tani 45, Spreader mbili zenye urefu wa futi 40, Spreader mbili za urefu wa futi 20.

Mradi huo wa awamu ya kwanza ulishakamilika kwa asilimia 100 na meli kubwa zimeanza kuingia na kutia nanga kwenye eneo la maegesho.

Julai 30, 2020, TPA ilisaini mkataba na Mkandari M/S China Habour Engineering Company (CHEC), ikiwa ni awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari ya Tanga, ambapo kazi ilianza rasmi Disemba 16, 2020.

Mradi huo uligharamiwa na Serikali kupitia TPA, chini ya Wizara ya Uchukuzi. Uligharimu Shilingi bilioni 256.8 na hivi sasa umeshakamilika kwa asilimia 100, hivyo kuwezesha meli kubwa kufunga gatini.

Mrisha anasema, maboresho hayo kumeimarisha utendaji kazi bandarini na kuboresha magati mawili yenye urefu wa mita 450, kuongeza mita 50 (mashariki) na mita 92 (magharibi) kuelekea baharini na kuongeza kina cha maji kutoka mita 3 hadi mita 13. Hatua. hizo zinaijengea uwezo bandari ya Tanga kuhudumia meli kubwa gatini.

*Inaendelea uk 12*



*Shehena zikishushwa kwenye bandari ya Tanga.*

# BILIONI 429 ZA UBORESHAJI...

*Inatoka uk 11*

**Ushiriki wa wazawa**

Taarifa ya Mhandisi Mshauri wa inaeleza kuwepo ajira Wahandisi wazawa wanne na kwa upande wa kada nyingine, aliajiri wafanyakazi watatu wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Kwa upande wa Mkandarasi Mjenzi, wafanyakazi wazawa 151 mpaka 581 wa kada mbalimbali waliajiriwa kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi huo.

Kabla ya kujengwa gati hili, bandari hiyo ilihudumia shehena isiyozidi tani 750,000 kwa mwaka, lakini baada ya upanuzi, uwezo huo umeongezeka kufikia tani 3,000,000.

Sehemu ya shehena zinazoingizwa nchini na nchi jirani kupitia bandari ya Tanga ni malighafi za viwandani kama pet-coke, clinker, ammonium nitrate, sulphur, vipuri vya magari, mitambo ya viwandani, petroli na dizeli.

Kwa upande wa zinazosafirishwa nje ya nchi ni pamoja na mazao ya misitu, shaba, kahawa, mkonge, viungo na macadamia.

Mathalani, katika kipindi cha 2019 hadi 2024, shehena iliyohudumiwa bandarini hapo iliongezeka kutoka tani 470,611 hadi tani 1,191,480 ikiwa ni sawa na asilimia 27.2 kwa mwaka.

**Meli za kimataifa na mwambao**

Kwa upande wa meli za kimataifa na mwambao zilizohudumiwa, zimeongezeka kutoka 118 mwaka 2019 hadi 307 mwaka 2024, ikiwa ni sawa na asilimia 31.6 kwa mwaka.

**Ongezako la mapato**

Kwa kipindi cha 2019 hadi 2024, mapato yanayotokana na huduma za bandari hiyo yameongezeka kwa wastani wa asilimia 17 kwa mwaka, lakini kwa 2023/24, kiasi hicho kilipanda kufikia asilimia 74 ikilinganishwa na milivyokuwa 2022/23.

Pia, kuna ongezeko la shehena kutoka tani 890,901 mwaka 2022 hadi tani 1,191,480 mwaka 2024, muda wa kuhudumia meli umepungua kutoka siku tano hadi mbili na ongezeko la mapato kwa asilimia 74.1 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023.

Kwa ujumla, maboresho ya bandari ya Tanga ni chachu ya maendeleo na ufunguo kwa ukanda wa kaskazini. TPA inapaswa kuendelea kusimamia vema nyanja ya bandari ishiriki katika kuzalisha na kuirudishia Serikali faida, kabla ya muda wa marejesho ya gharama zilizowekezwa.

Aidha, Serikali na wadau wengine kama Sekta Binafsi waendelee kutekeleza mipango ya kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa nchi kavu hasa reli na kuwekeza katika kilimo cha biashara na viwanda katika mikoa inayozunguka Bandari ya Tanga ili kuchochea matumizi ya Bandari ya Tanga.



*Mwonekano wa bandari ya Tanga.*



*Meli ikiwa imetia nanga katika Bandari ya Tanga.*

# DARAJA LA MTO PANGANI KUIMARISHA MIUNDOMBINU NA UCHUMI KANDA YA PWANI

**Na Martine Kamote, PANGANI**

Serikali ya Tanzania imezindua mradi mkubwa wa ujenzi wa daraja la kisasa litakalounganisha mikoa ya Tanga na Pwani.

Daraja hili litakalojengwa juu ya Mto Pangani na lenye urefu wa mita 525, linatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi na uchumi wa kanda ya pwani ya bahari ya Hindi, mikoa ya kaskazini na nje ya nchi.

Mradi huu unaogharimu Shilingi bilioni 82.19, unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36 (miaka mitatu).

### Manufaa

Daraja la mto Pangani ni sehemu muhimu ya barabara kuu ya Afrika Maashariki kuanzia Tanga - Pangani – Saadani - Bagamoyo, itakayorahisisha usafiri kati ya mikoa ya Tanga na Pwani.

Hadi sasa, watu wengi wanalazimika kuvuka Mto Pangani kwa kutumia boti au njia mbadala, jambo ambalo limekuwa likichukua muda mrefu na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Kukamilika kwa daraja la mto Pangani kutawasaidia watu katika urahisi wa kusafiri kwa usalama na haraka kutoka upande mmoja wa mto hadi mwingine.

### Miundombinu na Maendeleo

Kwa upande mwingine, daraja la mto Pangani ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya kuboresha miundombinu ya usafiri, hasa kwa kuunganisha mikoa mbalimbali.

Kupitia daraja hilo, huduma za kibiashara zitakuwa rahisi na gharama nafuu kwa wakazi wa maeneo ya Tanga, Pangani, Bagamoyo na Saadani.

Pia, wananchi wataweza kufika kwenye maeneo ya biashara na huduma kama vile masoko, hospitali, ofisi za halmashauri na benki kwa urahisi, jambo ambalo litachochea uchumi wa maeneo hayo.

Zaidi ya hayo, mradi huo unatarajiwa kuchochea shughuli za uzalishaji mali na biashara katika maeneo ya pembezoni, kwani wafanyabiashara watapata fursa ya kufikia masoko kwa haraka na kwa urahisi.

Hatua hiyo itasaidia kuboresha hali ya maisha kwa wakazi wa ukanda wa Pwani, na kuongeza nafasi za ajira katika sekta mbalimbali kama vile ujenzi, usafiri, na biashara.

### Usalama na huduma

Kwa kutekeleza mradi huo wa daraja la Mto Pangani, Serikali inalenga kuhakikisha usalama wa watu wanaosafiri kutoka upande mmoja wa mto hadi mwingine.

Pamoja na daraja hilo, watu watakuwa na fursa ya kutumia barabara salama za kisasa ambazo zitapunguza ajali na changamoto za usafiri zinazokumba maeneo hayo.

### Mwisho wa safari ndefu, usumbufu

Ujenzi wa daraja hilo pia unalenga kutatua changamoto za muda mrefu wa usafiri, zinazowakumba wananchi.

Watu wengi ambao wamekuwa wakilazimika kutumia boti kuvuka mto Pangani kwa ajili ya shughuli za kibiashara, huduma za kiofisi na kusafiri kwenda maeneo mbalimbali ya kanda, watapata urahisi wa kusafiri bila ya kupoteza muda.

Hali hiyo itasaidia kuboresha maisha yao na kuongeza tija katika shughuli zao za kila siku.

Mradi wa ujenzi wa daraja la Mto Pangani ni hatua muhimu katika kuboresha miundombinu na uchumi wa mikoa ya Tanga na Pwani.

Utakapokamilika, utarahisisha usafiri, kupunguza gharama za kibiashara, na kuchochea maendeleo katika maeneo ya pembezoni.

Aidha, daraja hilo litakuwa ni kielelezo cha maendeleo endelevu na matumizi bora ya rasilimali za taifa katika kuboresha huduma za kijamii na uchumi.



*Daraja la Mto Pangani*

# UBORA WA MIUNDOMBINU, ELIMU NA MAZINGIRA VINAVYO



*Baadhi ya miundombinu ya mabweni ya Shule ya Sekondari ya Miles and Kimberly*

**Na Nassoro Rashid, MKINGA**

Kutoka shule isiyokuwa na miundombinu madhubuti ya majengo kwa miaka 16, wakati huo ikiitwa Shule ya Sekondari Mapatano, sasa mambo yamebadilika. Ujenzi mpya umeifanya kuwa bora na ya kisasa kwa maisha na kujifunza.

Ikiwa imejengwa katika kata ya Mapatano wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, shule hiyo ilipata ufadhili kutoka taasisi ya Abbott Fund yenye makao yake Marekani, kusaidia ujenzi wa shule hiyo kwa kuhusisha ukarabati wa majengo yaliyokuwepo na kujenga mengine mapya, ikawa asili ya mabadiliko hayo.

Mabadiliko ya miundombinu yaliyotokea, yakaelekezwa hadi kubadili jina kutoka Mapatano, sasa inaitwa Shule ya Sekondary ya Mile and Kimberly Whites na ilizinduliwa rasmi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, Oktoba 1, 2024.

Shule ya awali ilijengwa mwaka 2008 kwa nguvu za wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya kuhakikisha kila kata nchini inakuwa na shule ya sekondari. Ilisajiliwa kwa namba S3810 na kupata idhini ya kuwa na kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mikondo miwili.

Takwimu zilizopatikana halmashauri ya wilaya ya Mkinga zinaonesha kuwa, Mwaka 2022, Shule ya Sekondari Mapatano ilikuwa na wastani wa wanafunzi 400, lakini haikuwa na miundombinu toshelezi kama vile madarasa, nyumba za walimu, maabara, ofisi za walimu na vyoo kwa matumizi ya wasichana, wavulana na watumishi.

Hata hivyo, shule hiyo iliendelea kuwahudumia watoto waliochaguliwa kutoka katika kata ya Mapatano na kutoka kata nyingine za jirani.

Hali hiyo ikawa kichocheo cha ushawishi kwa raia wawili wa Marekani, Miles White na mke wake, Kimberly Whites, walipoona kuwa watoto wanaomaliza shule ya msingi wanaweza wakakosa fursa ya kuongeza kiwango cha elimu,s wakaamua kufadhili upanuzi na uboreshaji wa Shule ya Sekondari Mapatano.

Ufadhili huo uliopitia shirika lisilokuwa la kiserikali la Abbott Fund, ukahusisha ukarabati wa majengo yote yaliyokuwa yakitumika, kisha kujenga mengine mapya kwa ajili ya kidato cha tano na sita.

Mradi huo katika ujumla wake, umegharimu Shilingi bilioni 12 katika uboreshaji wa miundombinu na kuifanya kuwa inayowezesha mazingira mazuri ya kujifunza na kujifunzia.

Majengo yaliyokarabatiwa ni madarasa 14 na maabara za fizikia, kemia, baiolojia ambazo zote zilibadilishwa paa, rangi, madirisha, milango, sakafu kuwekewa tiles na kuwekewa huduma ya umeme, maabara ya kilimo, nyumba mbili za walimu zilibadilishwa madirisha na kupakwa rangi, ofisi za walimu zilibadilishwa paa, madirisha, milango, kuwekewa umeme na tiles,

Majengo mapya yaliyojengwa ni la utawala, maktaba, ofisi ya mkutubi, jiko, bwalo, ukumbi wa mikutano, madarasa nane ya kidato cha tano na sita, nyumba nne (2 in 1) za walimu, nyumba mbili za matron na patroni, nyumba ya kupumzisha wagonjwa ikiwa na vifaa vya huduma ya kwanza na kichomea taka.

vya wavulana, mabweni manne, kati yao mawili ya wasichana na mawili ya wavulana yenye

***Inaendelea uk 15***

# CHOCHEA UTULIVU SEKONDARI YA MILES AND KIMBERLY WHITE




*Jengo la maktaba*

***Inatoka uk 14***

uwezo wa kulaza wanafunzi 112 kwa kila moja. Ujenzi wa majengo yaliyokarabatiwa na kujengwa umezingatia hali ya watu wenye mahitaji maalum.

Pamoja na majengo hayo, mradi huo ulihusisha utoaji vifaa yaani kompyuta 20 na mfumo wa data, kabati maalum za kuhifadhi vitabu, vitabu 7,600 vya kiada na ziada kutoka Taasisi ya Elimu (TIE), viti na meza za walimu na wanafunzi, fulana za wanafunzi na wafanyakazi, mabegi, madaftari, calculator, rula, kalamu za wino, penseli, mikebe na vifutio.

**Idadi ya wanafunzi na tahasusi**

Kwa sasa Shule ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne wapatao 563 na kati yao, wasichana 272 na wavulana 291. Kidato cha tano wanafunzi 137 na kati ya 186 waliopangwa, wasichana ni 68 na wavulana 69. Aidha tahasusi zilizopo shuleni kwa sasa ni PCM, PCB, CBA na HGL kwa kidato cha tano. Kwa hiyo jumla ya wanafunzi wote katika shule hiyo kuanzia kidato cha kwanza hadi cha tano ni 710, yaani wasichana ni 340 na wavulana ni 360.

**Ufadhili wa walimu**

Katika kuhakikisha wadau wa maendeleo wanaunga mkono juhudi za Serikali ya Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan kupata matokeo bora kwa wanafunzi, Abbott Tanzania imewalipia walimu tisa wanajitolea kwa sasa shuleni hapo. Kati ya hao walimu wa masomo ya sayansi ni saba wa sanaa ni wawili.

**Dk Biteko aizindua kwa kutoa onyo**

Akiizindua shule hiyo, Mhe Dk Biteko aliwataka wakazi wa Tanga hususani Mkinga, kuitunza miundombinu yote



*Darasa la TEHAMA*

inayowawezesha watoto kupatia elimu bora shuleni hapo.

Mhe Dk Doto Biteko, akawaonya watu wanaoshiriki vitendo vinavyowanyima watoto haki ya kuendelea na masomo, na kusema wanakabiliwa na adhabu ya jela na aibu isiyofutika kwenye maisha yao.

Alisema jitihada zinazofanywa na Serikali na wahisani ikiwemo Abbott Fund, kuboresha miundombinu ya elimu, zinapaswa kuungwa mkono na jamii, kwa kuepuka na kudhibiti vitendo vya dhuluma na unyanyasaji vinavyochangia kupora haki za mtoto ikiwemo kupata elimu.

“Ni jukumu la jamii kuhakikisha kila mtoto anapata elimu, kuepuka na kudhibiti vitendo vikiwemo vya kumharakisha (mtoto) kwenye maisha ya baadaye kama vile kumuingiza kwenye ndoa za utotoni,” alionya.

Pia, Mhe Dk Biteko aliwahimiza watoto kuepusha vishawishi, badala yake watumie kipindi cha ujana wao kupata elimu, maarifa na ujuzi hivyo kujiweka katika nafasi nzuri ya kuwa viongozi na wazazi bora wa baadaye.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Abbott, Robert Ford alisema Wakfu huo ulianza kujihusisha na miradi ya maendeleo mkoani Tanga mwaka 2001, ‘ikijikita’ zaidi katika sekta ya elimu, kwa kutambua kuwa ndio msingi wa nyanja za kijamii.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Zainab Katimba, alisema kwa kipindi cha kufikia Juni 2024, Serikali ilishatumia Shilingi trilioni 3.43 kuboresha miundombinu ya elimu chini.

# TANGA 'KINARA' KILIMO CHA MKONGE TANZANIA

**Na Ester Mbusi, TSB**

MKONGE ni zao maarufu la kibiashara, hususani katika mikoa ya ukanda wa Pwani, Kaskazini na Ziwa Viktoria. Takwimu za Bodi ya Pamba (TSB) zinaonesha kuwa zao hilo linalostawi kwenye mikoa 18 nchini.

Mikoa hiyo ni Tanga, Morogoro, Pwani (Chalinze na Kibaha), Kilimanjaro, Manyara, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Geita, Kagera, Lindi, Kigoma, Tabora, Katavi, Ruvuma na Mtwara.

Kutokana na umuhimu wa mkonge nchini, Serikali ililiongeza kwenye mazao ya kimkakati ambapo mwaka 2020, Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa, alibainisha azma ya Serikali kurudisha na kuimarisha mazao muhimu ya kimkakati ikiwamo mkonge.

**Uzalishaji Mkonge**

Katika kuhakikisha uzalishaji unaongezeka kufikia lengo la Serikali kuzalisha tani 230,000 ifikapo 2025/26, TSB imejiweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuongeza hamasa kwa wakulima kushiriki kilimo cha zao hilo ambapo Tanga imeendelea kuongoza kwa uzalishaji.

Mwaka 2021 hadi 2024, uzalishaji wa singa za mkonge kitaifa uliongezeka kutoka tani 39,484.27 mwaka 2021 hadi kufikia tani 61,215.55 mwaka 2024 sawa na asilimia 55.

Tanga imeendelea kuongoza katika uzalishaji wa mkonge nchini kwa tani 34,445.21 mwaka 2024 sawa na asilimia 56.27 ya zao hilo nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TSB, Saddy Kambona alisema uzalishaji kimkoa umeongezeka kutoka tani 26,512.12 mwaka 2021 hadi tani 34,445.21 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la tani 7,933.09 sawa na asilimia 30.

Alisema, kwa mkoa wa Tanga, wilaya ya Korogwe imekuwa ikiongoza katika uzalishaji, ikifuatiwa na wilaya za Muheza na Pangani.

Pia alisema upandaji wa mkonge mkoani Tanga umeongezeka kutoka hekta 3,578.20 mwaka 2021 kufikia hekta 7,819.35 mwaka 2024 (asilimia 118.52).

Kambona alisema ngezeko hilo limechangiwa na hamasa kubwa ya Serikali katika uwekezaji wa kilimo cha mkonge kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa, ugawaji wa mbegu bure kwa wakulima wadogo na wapya wa mkonge.

Kwa mujibu wa Kambona, hadi kufikia 2024 jumla ya mbegu zaidi milioni sita ziligawiwa kwa wakulima wa wilaya za Mkinga, Handeni, Pangani, Korogwe, Lushoto, Muheza, Kilindi na Tanga.

**Ongezeko la wakulima wa mkonge**

Mfumo wa kilimo cha mkonge kwa wakulima wadogo nchini umeendelea kukua, ambapo mkoani Tanga pekee, wakulima wadogo wa zao hilo wamefikia 9,871 kwa 2024 kutoka wakulima 3,197 waliokuwepo 2021.

Kambona alisema wakulima wengi wanapatikana katika wilaya za Korogwe, Muheza, Mkinga, Lushoto, Handeni, Pangani na Kilindi.

**Mitambo ya kusindika mkonge**

Kambona anaitaja mitambo hiyo kuwa ni korona, kayamba na press ambayo imeongezeka kwa kipindi cha miaka minne kutoka korona 47 mwaka 2021 kufikia 57 mwaka 2024.

Alisema, hali hiyo inatokana na hamasa iliyoratibiwa na TSB na Serikali kwa ujumla, katika uwekezaji wa kilimo cha mkonge kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa.

Kambona alisema katika kurahisisha uchakataji mkonge kufanyika kwa ufasaha, TSB

*Inaendelea uk 17*



*Zao la mkonge.*



*Uzalishaji wa katani ukifanyika kwenye kiwanda cha kampuni ya Sisalana Tanzania ambacho ni kampuni Tanzu ya NSSF.*

***Inatoka uk 16***

imenunua gari la kuchimba visima vya maji kwa ajili ya kuwezesha uendelezaji wa mashamba makubwa ya pamoja, na kununua mashine ya kuchakata mkonge inayoendelea kusimikwa kwenye kijiji cha Taula wilayani Handeni.

**Kuchangia kwa pato la fedha kigeni**

Kwa kipindi cha 2021 hadi 2024, mkonge mkoani Tanga umechangia zaidi ya Dola milioni 131.7 za Marekani. Kambona anasema hayo ni mafanikio makubwa kwa zao hilo.

Anasema kwa sasa zao lina mahitaji makubwa kwenye masoko ya nje ya nchi, yaliyochangiwa na matumizi mapya ya singa. Mkonge unahitajika kwenye viwanda vya ujenzi, utengenezaji wa magari na ndege.

**Ajira**

Kambona anasema ajira rasmi na zisizo rasmi kitaifa kupitia mkonge, zimeongezeka kutoka 302,838 mwaka 2021 hadi 497,453 kwa mwaka 2024 huku Tanga ikiongoza kwa idadi kubwa ya takribani asilimia 60 ya ajira zote katika zao hilo.

Anasema, hatua hiyo inachangiwa na kuongezeka kwa mashamba ya mkonge na viwanda, hali iliyofanya kuongezeka kwa wafanyakazi wengi katika mnyororo wa thamani wa zao la hilo.

**Viwanda vya kuongeza thamani**

Kambona anasema kuna ongezeko la kiwanda kimoja cha kuongeza thamani bidhaa za mkonge kilichojengwa wilayani Korogwe.

“Kwa sasa Tanga ina viwanda vinne vya kuongeza thamani bidhaa za mkonge, viwili vipo, Muheza na Korogwe kiwanda kimoja kila wilaya”.

**Kituo Atamizi cha Mkonge**

Ni katika kipindi hicho cha miaka minne, TSB imefanikiwa kuanzisha Kituo Atamizi cha Mkonge mkoani Tanga, kwa lengo la kutoa fursa kwa vijana na watu wenye ulemavu kujifunza utengenezaji wa bidhaa za mkonge, kuongeza wigo wa matumizi ya mkonge na bidhaa zake pamoja na kuongeza ajira.

Anasema kituo hicho kilichozinduliwa Oktoba 5, mwaka jana na Waziri wa Kilimo, Mhe Hussein Bashe, kina watu 31 ambapo wanawake 18, wanaume 8, wakufunzi wanne na msimamizi wa kituo mmoja

# HOSPITALIYABILIONI8INAVYOBORESHAAFYAHANDENI



Hospitali ya Wilaya iliyopo Halmashauri ya Wilaya Handeni.

**Na Cyprian Luanda, HANDENI**

Kutoka kusafiri umbali za zaidi ya kilomita 50 kufuata huduma za afya mjini Handeni, hospitali ya wilaya iliyopo Mkata, makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Handeni, inatoa jawabu la ubora, unafuu na upatikana haraka na wa uhakika wa huduma za afya kwa wakazi wake.

Awali, wakazi wa halmashauri hiyo walisafiri umbali mrefu kutoka maeneo tofauti, kwenda mjini Handeni kupata huduma ambazo hazitolewi kwenye zahanati na vituo vya afya vilivyopo kwenye ngazi za chini kwenye jamii.

Hatua ya kusafiri umbali mrefu ilisababisha kadhia tofauti, ikiwemo ya wananchi hasa wa kipato cha chini, kushindwa kuzifikia huduma zinazotolewa kwenye ngazi ya hospitali ya wilaya kwa haraka.

Kwa upande mwingine, waathirika wa ajali zilizotokea kwenye barabara ya Chalinze – Segera, walilazimika kusafirishwa umbali mrefu kwenda hospitali ya mkoa wa Pwani – Tumbi iliyopo Kibaha.

Lakini sasa halmashauri hiyo imepata hospitali ya wilaya hiyo iliyogharamiwa na Serikali na ufadhili wa taasisi ya Islamic Foundation.

Hospitali hiyo ipo kwenye kijiji cha Mkata Mashariki, kata ya Mkata, tarafa ya Mazingara, kandoni mwa barabara kuu ya kutoka jijini Dar es Salaam kwenda mikoa ya kaskazini hususani Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

*Inaendelea uk 19*



Sehemu ya vifaa tiba vya kisasa kwenye Hospitali ya Wilaya Handeni.

*Inatoka uk 18*

### Utekelezaji

Ujenzi wa hospitali hiyo ulianza 2013 -2014 kwa kuanzia na jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kupitia fedha za Serikali Kuu. Mpaka sasa, majengo yaliyokamilika ni OPD, dharula, bohari ya dawa, maabara, mionzi, mama na mtoto, wodi ya wanaume, wodi ya wanawake, upasuaji, jengo la kufulia, jengo la kuhifadhia maiti, wodi ya watoto, kichomea taka na njia za kupita.




*Jengo la utawala la Hospitali ya Wilaya Handeni.*

### Utoaji wa Huduma

Juni 1, 2023, hospitali hiyo ilianza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD), wagonjwa wa ndani (IPD), kujifungua, maabara, upasuaji, ultra sound na X RAY, dawa, dharura, kuhifadhi maiti, kliniki ya watoto na wazazi (RCH), kinywa na meno, physiotherapia (mazoezi tiba) na watoto njiti (NICU).



### Watumishi

Serikali imeajiri watumishi wa afya 76 ikiwa ni asilimia 38 ya 200 wanaohitajika wa kada za udaktari, uuguzi, ufamasia, wataalam wa mazoezi tiba na maabara.

Pia hospitali hiyo ina watumishi 10 wa mikataba (vibarua) wanaolipwa kwa kupitia makusanyo ya ndani ya halmashauri, ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wakazi wake.



*Huduma za vipimo kwenye Hospitali ya Wilaya Handeni.*

# ZIJUE FURSA ZA

Na Ester Mbusi, TSB

Mkonge ni zao mtambuka ambalo linachangia ukuaji uchumi na kipato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Miaka ya hivi karibuni, watu wengi wamehamasika kulima mkonge na kunufaika kwa njia mbalimbali ikiwamo ajira na uzalishaji bidhaa zinazotokana na mkonge, japo kuzitaja kwa uchache.

Mkoa wa Tanga ni wa kwanza kwa kuanzisha kilimo cha mkonge. Zao hilo liliingizwa nchini na mtaalamu wa kilimo (Agronomist), Dk. Richard Hindorf kutoka kisiwa cha Yucatan nchini Mexico mwaka 1893.

Tangu wakati huo, mkonge umeendelea kuenea katika mikoa mingine 18 nchini yenye ardhi inayokubali zao hilo.

Pamoja na mambo mengine, ziko fursa nyingi ambazo watu wanaweza kunufaika nazo kupitia zao la mkonge, ikiwamo uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na zao hilo, uzalishaji mbegu, mashine za kuchakata mkonge na nyingine nyingi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Zao wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Olivo Mtung'e anasema wawekezaji au mtu mmoja mmoja wanaweza fursa hizo wakafanikiwa kwani mkonge una fursa nyingi kulingana na mahitaji husika.

Anasema kwa sasa mahitaji ya mashine za kuchakata mkonge yaani korona ni makubwa ambapo wawekezaji wanaweza kutumia fursa hiyo kuwekeza ili kukidhi mahitaji ya wakulima wa zao hilo wanaoongezeka siku hadi siku.

"Wilaya mbalimbali hapa Tanga zina upungufu wa mashine za kusindika mkonge, hivyo wanahitajika wawekezaji wenye uwezo wa kuwekeza mashine hizo ili kuwasaidia wakulima waliopo kwenye wilaya za mkoani Tanga,'' amesema.

Anaongeza, "lakini pia kuna ubunifu wa bidhaa mbalimbali za mikono kwa kutumia teknolojia rahisi ambayo inafahamika lakini haijatumika sana hapa Tanga, viwanda vya kutengeneza kamba, magunia nakadhalika," anasema Mtung'e.

Kuhusu upatikanaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo cha mkonge, anasema ardhi inayofaa ipo kwenye wilaya za mkoani Tanga na kwamba TSB inaendelea kutoa ushauri na wataalamu wake ili mkulima alime kilimo chenye tija.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Masoko na Uhamasishaji wa TSB, David Maghali anasema zao la mkonge linatoa fursa nyingi na kwamba linahitajika kwa wingi kwenye soko la dunia.

Anasema manufaa ya mkonge yanaanzia kwenye jani la zao hilo hadi mizizi yake. Hivyo zao hilo likitumiwa vizuri itainua uchumi wa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla.

Maghali anasema, "shina la mkonge linatoa asali lakini pia linatoa spirit, wenzetu Wabrazil wanatengeneza pombe inaitwa tequila.''

Anaongeza, "shina la mkonge linatengeneza mlingoti unaotumika kwa ajili ya ujenzi na mizizi ya shina inatengeneza mbolea inayotumika katika mazao mbalimbali.''

Kilimo cha mkonge ni fursa pana kutokana na ukweli kwamba, uzalishaji wake duniani uko chini ikilinganishwa na mahitaji wakati ambapo Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji duniani.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Tanzania ilizalisha tani 48,000 za mkonge kwa mwaka jana wakati lengo ni kuzalisha tani 120,000 kwa mwaka ifikapo 2025. Hivyo nguvu kubwa ya uwekezaji kwenye kilimo cha zao bado inahitajika.

Maghali anasema, uzuri wa mkonge unastahimili ukame ikilinganishwa na mazao mengine, hivyo anashauri kufanyika uwekezaji usiotilia shaka mabadiliko ya hali ya hewa.

# MKONGE TANGA

Anasema, "uzuri wa mkonge unastahimili sana ukame, hautaki sehemu ambayo maji yanasimama. Hali hiyo ipo kwa wingi kwenye maeneo ya mkoa wa Tanga tunapowahimiza kuja kuwekeza kwenye kilimo cha zao hili," anasema.

Kuhusu soko la mkonge, Maghali anasema, "kuna masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi, wale ambao wanazalisha kwa kiasi kidogo kwa maana kuna viwanda vya kuzalisha kamba, gunia na mazulia. Kwa hiyo hao ndiyo wanunuzi wa mkonge wa wakulima hawa wadogo.''

Pia anasema kuna masoko ya nje kwa wale wakulima ama wafanyabiashara wanaoweza kuuza tani 26-27 na kuendelea kwa mara moja na kuwa usafirishaji wake unafanyika kwa kutumia kontena lenye urefu wa futi 40.
Ameyataja masoko ya mkonge nje ya nchi kuwa ni China, Saudi Arabia, Nigeria, Japan, Misri, Morocco, Hispania na Guinea.

Katika kuhamasisha kilimo cha mkonge mkoani Tanga na Tanzania kwa ujumla, Maghali anasema; "TSB imejipanga kuongeza idadi ya miche kwa wananchi ambao wako tayari kulima mkonge na wanatakiwa ofisi za bodi hiyo kuhusu uhitaji wao wa miche."

Sifa za kupatiwa mbegu
Maghali anasema kuna sifa mkulima anatakiwa kuwa nazo ili kupatiwa mbegu za mkonge.

Anasema anayestahili kupatiwa mbegu ni yule aliyeandaa eneo tayari kwa kilimo cha mkonge, kwa sababu mbegu zinapopelekwa zinatakiwa zikae ndani ya wiki mbili kabla ya kupandwa.

Kwa hiyo, anasema, mtu anapoomba mbegu lazima wataalamu walitembelee eneo husika (shamba) ili wakajihakikishie eneo ili mbegu zitakazopelekwa zisije kuharibika ama kukosa matumizi.

Kwa hiyo, anasema, mtu anapoomba mbegu lazima wataalamu walitembelee eneo husika (shamba) ili wakajihakikishie eneo ili mbegu zitakazopelekwa zisije kuharibika ama kukosa matumizi.



*Uzalishaji ukifanyika kwenye kiwanda cha kampuni ya Sisalana Tanzania ambacho ni kampuni Tanzu ya NSSF.*

# WANAWAKE HANDENI WASEMA 'NDIYO', WAMTUNUKU RAIS SAMIA



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian akiwa amebeba Tuzo ya Heshima iliyotolewa na watumishi wanawake wa halmashauri ya wilaya ya Handeni kwa Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan*

**Na Mashaka Mgeta, OMM – TANGA**

Ni kama kauli ya pamoja wanapotamka 'ndiyo' kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dk Samia Suluhu Hassan, kwa mafanikio yanayowagusa wanawake watumishi wa umma katika halmashauri ya wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

Watumishi hao wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Saitoti Stephen wametafakari kwa kina kuhusu mazingira bora mahali pa kazi, wingi, kasi ya utekelezaji na ukubwa wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika kipindi cha utawala wa Mhe Rais Dk Samia.

Wakaona wasikae kimya, bali kukutana pamoja na kutuma salaam za pongezi kwa Mhe Rais Dk Samia, kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian, akifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe Albert Msando na kumkabidhi tuzo hiyo jana.

Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Rachel Mbelwa, akasema wameamua kumpongeza Mhe Rais Dk Samia kutokana kasi ya maendeleo, ukuaji uchumi, uboreshaji huduma za jamii na mazingira bora mahali pa kazi.

Mhe Balozi Dk Batilda, akawaasa Watanzania kusimamia ukweli wa mafanikio makubwa yanayotokana na uongozi wa Mhe Rais Dk Samia, na kuepuka hulka ya kuyabeza kwa vile Serikali ya Mhe Rais Dk Samia imefanya mambo makubwa katika uboreshaji wa huduma za kijamii, na kutekeleza ahadi zilizotolewa kuhusu miradi ya maendeleo.

Ametoa mfano kuwa, katika bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali imeidhinisha takribani Shilingi trilioni 2.6 kwenye miradi ya sekta mbalimbali mkoani humo ikiwemo elimu, afya na miundombinu.

Mhe Balozi Dk Batilda amesema pia kuwa uboreshwaji wa bandari ya Tanga, ujenzi wa miradi ya kimkakati kama vile bomba la mafuta na barabara ya Tanga - Pangani nadi Bagamoyo, ni miongoni mwa mafanikio ya utawala wa Mhe Rais Dk Samia.

**WAHESHIMU UTENDAJI KAZI WA RC, RAS NA DAS**

Wanawake watumishi hao wa halmashauri ya wilaya ya Handeni, wakasema wanatambua utendaji kazi bora wa viongozi wanawake waliopo mkoani humo, na kwa niaba yao wakatoa tuzo kwa watatu miongoni mwao.

Waliotunukiwa tuzo hizo ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda, Katibu Tawala Mkoa (RAS) wa Tanga, Pili Mnyema na Katibu Tawala Wilaya (DAS) ya Handeni, Magreth Killo.



*Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Rachiel Mbelwa.*

# JENGO LA UTAWALA LINAVYOHARAKISHA UTOAJI HUDUMA HANDENI MJI

**Na Job Karongo, Handeni Mji**

Ujenzi wa jengo la Utawala katika halmashauri ya Mji Handeni mkoani Tanga, umekamilika na kutumika rasmi, ikiwa ni hatua muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, na mazingira bora ya kazi kwa watumishi wa umma.

Jengo hilo ambalo ujenzi wake ulianza Oktoba 2017, lilijengwa chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) kwa gharama ya Shilingi 3,619,007,387, ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Ujenzi huo ulikuwa na mkataba wa miezi 24 (miaka miwili), huku ukilenga kuboresha mazingira ya utendaji wa halmashauri na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi mjini Handeni.

Tofauti na ilivyokuwa kwenye majengo ya awali, jengo hilo jipya la utawala lina nafasi ya kutosha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiutawala.

''Kukamilika kwake kumetoa fursa kwa wananchi kupata huduma kwa urahisi zaidi, huku watumishi wakifanya kazi katika mazingira bora na yenye ufanisi,'' anasema xxxxx.

Hadi kufikia Januari 2025, halmashauri ya Mji Handeni ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 3,850,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo, ambapo shilingi 3,609,338,934.57 zimetumika, ikiwa ni sawa na asilimia 94 ya fedha zote zilizotolewa kwa mradi huo.

Mbali na jengo hilo, halmashauri pia inaendelea na ujenzi wa uzio, mandhari ya nje na mgahawa wa watumishi.

Hadi Makala haya yanaandikwa, ujenzi wa uzio ulikuwa asilimia 40, mandhari (landscaping) asilimia 98 na mgahawa uko katika hatua ya asilimia 28 ya utekelezaji wake.

Licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana, changamoto ya kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi iliongeza gharama za utekelezaji wa mradi.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, halmashauri ilichukua hatua ya kununua vifaa vya ujenzi kwa mkupuo moja kwa moja kutoka viwandani, jambo ambalo limesaidia kupunguza gharama na kuhakikisha kuwa vifaa vinapatikana kwa wakati.

Halmashauri ya Mji Handeni imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinapatikana kwa wakati.

Uwekezaji hu unaakisi dhamira ya Serikali katika kuboresha miundombinu ya utawala na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.




*Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Handeni*

# JIOGRAFIAYATANGAINAVYOCHOCHEAUWEKEZAJI

**Na Mbarouk Yusuf, TANGA**

Tanga ni moja ya mikoa nchini Tanzania iliyo na fursa nyingi za uwekezaji katika sekta tofauti, kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mazingira ya mkoa ulivyo kijiografia.


Mkoa huu upo kwenye eneo lenye bahari ya Hindi na hivyo kuifanya bandari ya Tanga iliyoboreka, kuwa kitovu cha kupokea mizigo inayoingia kwenda kwenye wilaya zake, mikoa jirani ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Pwani na nchi jirani ya Kenya.

Tanga inabaki kuwa eneo bora kijiografia lililopo takribani kilomita 100 kufika bandari ya Mombasa nchini Kenya, kilomita 350 kwenda Mlima Kilimanjaro ulio mrefu kuliko milima yote barani Afrika na kilomita 360 hadi kufika bandari ya Dar es Salaam.

Kwa upande wa usafiri wa anga, inachukua muda wa nusu saa kusafiri kwa ndege kutoka Tanga hadi visiwani Zanzibar; hali inayotoa mazingira bora ya kiuchumi na kijamii kwa wafanyabiashara na watoa huduma wanaowekeza Tanga.

Lakini pia ipo meli ya kisasa ya Zan Fast Ferries inayofanya safari zake kati ya Tanga, Pemba, Zanzibar na Dar es Salaam, na hivyo kuwa kiunganishi kikubwa na kizuri kwa mafungamano ya kijamii na kibiashara kati ya wakazi wa maeneo hayo na mengine ya jirani.

Maana yake rahisi ni kwamba, shughuli za kiuchumi na mwingiliano wa watu kutoka maeneo hayo, utachagizwa kasi ya ukuaji wa uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa bidhaa na huduma zinazowekezwa mkoani Tanga.




Ni kutokana na jiografia ya mkoa wa Tanga, vipo vitu vingi vinavyoweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje ikiwemo kwenye sekta za kilimo,viwanda uvuvi,usafirishaji nakadhalika.

Kwa ujumla mkoa wa Tanga upo kwenye eneo zuri la kijiografia lililosheheni ardhi yenye rutuba na hali ya hewa nzuri kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma za jamii.

Kwa mfano, mwekezaji anayeweza kupanga na hatimaye kuwekeza kwenye kiwanda cha matunda hatakuwa amekosea kwani Tanga inahusika katika uzalishaji wa matunda ya aina mbalimbali yanayoingizwa kwenye masoko ya ndani ya nje ya nchi.

Uwepo wa miundombinu bora ya usafirishaji kwa njia ya bahari, anga, reli na barabara ni miongoni mwa nyenzo zinazomuwezesha mwekezaji kuwa na uhakika wa kufikisha mazao yake yakiwemo yanayotokana na kilimo kwenye masoko.

Kwa maana kila atakapozalisha mazao husika, upo uhakika wa usafiri wa kuyatoa shambani na kuyafikisha masokoni na kwenye viwanda vilivyo mkoani humo ama kwenye mikoa na nchi jirani.

Mbali ya uwepo wa ardhi ya kutosha na yenye rutuba nzuri, miundombinu bora ya usafiri na usafirishaji, viongozi wa Serikali mkoani Tanga chini ya Mkuu wa Mkoa, Mh Balozi Dk Batilda Burian, na Katibu Tawala Mkoa, Pili Mnyema, wakishirikiana na Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji, Wilaya na Jiji, wamepunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi, hivyo kuboresha hali ya utulivu na usalama.

# ZAN FAST FERRIES KUCHOCHEA UWEKEZAJI TANGA, INABEBA ABIRIA 615 KWA WAKATI MMOJA KWENDA PEMBA, ZANZIBAR

**Na Mwandishi Wetu, OMM TANGA**

Kwa mara ya kwanza, meli ya kisasa ya abiria inayofanya safari zake kutoka mjini Tanga kwenda Zanzibar, inatoa huduma zake kwa ufanisi na hivyo kuchochea urahisi wa watu kufika mkoani humu kwa shughuli mbalimbali ikiwemo uwekezaji.

Meli hiyo imekuja wakati ambapo mkoa wa Tanga wenye miundombinu bora ya usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kwa njia za barabara na anga, ulikuwa unazindua Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji mkoani humo.

Bila shaka, kuwepo kwa meli hiyo kukaongeza zaidi chachu ya viashiria vya mazingira bora yanayohusu sekta ya usafiri kwa wawekezaji, na kuunganishwa shughuli za biashara, uchumi na kijamii kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katibu Tawala Mkoa, Pili Mnyema, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya na wananchi wa jijini humo, wakashiriki uzinduzi wa safari za meli hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 615 kwa wakati mmoja.

Kuanza kwa safari meli hiyo ya Zan Fast Ferries inayomilikiwa na wazawa, ni matokeo ya mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara yaliyoboreshwa na Serikali ya Mhe Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Mhe Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kuwepo kwa meli hiyo yenye thamani za awali za uwekezaji wa takribani Shilingi bilioni 25, itachochea zaidi shughuli za kiuchumi na mahusiano ya kijamii kati ya wananchi wa Tanzania Bara, Zanzibar na mataifa jirani.

Pia, kwa vile changamoto ya ukosefu wa usafiri wa baharini kati ya maeneo hayo ni miongoni mwa kero zilizokuwepo kwa muda mrefu, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa meli hiyo ni ishara ya kuondokana na kero hizo.



*Meli ya Zan Fast Ferry*

# KWA KASI HII YA RAIS SAMIA, TANGA WAJIPANGE KWA UWEKEZAJI MKUBWA



*Ujenzi wa bomba la mafuta ukiendelea sehemu ya wilaya ya Handeni.*

**Na Amina Omar, TANGA**

NOVEMBA 15 hadi 17, 2024, iliingia kwenye historia ya mkoa wa Tanga, pale viongozi, wakazi na wadau wake wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi, walishiriki uzinduzi wa Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji mkoani humo.

Kabla yake, taarifa ilieleza kuwa tukio kama hilo lilifanyika miaka 10 iliyopita, na katika vipindi tofauti, uongozi wa mkoa wa Tanga umepitia hatua tofauti za kuelezea azma ya kuwepo kwa Mwongozo huo.

Uzinduzi wa Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji Tanga ukafanywa na Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa, aliyewakilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na uwekezaji ), Profesa Kitila Mkumbo , ikiwa ni sehemu ya Kongamano la Kutangaza Fursa za Uwekezaji mkoani Tanga.

Uzinduzi wa Mwongozo huo ukahitimisha kiu ya nyenzo iliyosubiriwa kwa muda mrefu katika kuchagiza ukuaji uchumi, maendeleo na ustawi wa wakazi wa Tanga.

Awali, kulijengeka dhana dhidi ya mkoa wa Tanga, kwamba hali ya uchumi wake imeporomoka, ikilinganishwa na miaka ya mwanzoni baada ya uhuru ambapo kulikuwa na rasilimali za uwekezaji kama viwanda, miundombinu ya usafiri, usafirishaji na mashamba ya mkonge.

Kwa hali hiyo, hali ya maisha ya wakazi wa Tanga ikaathirika, shughuli za uchumi na uzalishaji zikapungua, njia za mawasiliano zikafifia. Kukawa na athari kadha wa kadha kwenye nyanja za kiuchumi na kijamii.

Hata hivyo, umma umeshuhudia hatua kwa hatua, Serikali ikibuni na kutekeleza miradi inayogusa sekta mbalimbali zinazohusiana na uchumi, biashara, maendeleo na ustawi wa wananchi.

Uboreshaji wa njia kuu za uchumi kama vile miundombinu ya usafiri wa uhakika ikiwemo uwanja wa ndege, bandari na barabara bora zenye viwango vya lami kuunganisha wilaya zote za mkoa wa Tanga, mikoani na nchi jirani, umeonekana na hivyo kuibua, kukuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi.

Uwepo wa miradi mikubwa kama Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga, ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Sadaan – Bagamoyo na uborekaji wa huduma kwenye bandari ya Tanga, ni miongoni ishara nzuri za ukuaji wa uchumi wa mkoa huo.

Mageuzi ya kiutendaji na uwezeshaji kwenye taasisi za umma zinazoshughulikia nyanja za uchumi wa mkoa kama vile kilimo cha zao la mkonge, uanzishwaji wa mazao mapya ya kimkakati na huduma za jamii zinazohusiana na afya, maji, nishati nakadhalika ,yameifanya Tanga kuwa 'mpya' katika ukuaji wa uchumi wake.

Hii ni sawa na kusema, sasa mkoa wa Tanga umefunguka zaidi huku ikitiliwa maanani kwamba ndio mahali pekee palipo lango la kuu la Afrika Mashariki.

Fursa zilizo wazi na ambazo hazijadhirika kwa upana wake, zinatarajiwa kuibuliwa kupitia Kongamano la Kutangaza Fursa za Uwekezaji lililofanyika mkoani humo.

Miongoni mwa matarajio yaliyopo sasa ni kwa mdau kuendelea kutumia fursa ya mazingira bora ya amani, utulivu yaliyopo, kuibua biashara na huduma nyingi mkoani Tanga, hali itakayochangia pia ongeko la watu na muingiliano katika nyanja mbalimbali za kijamii.

Ni wazi sasa kwamba, Kongamano la Kutangaza Fursa za Uwekezaji mkoa wa Tanga lilikuwa ni fursa adhimu inayostahili kuendelea kuwatafakarisha wananchi, namna watakavyoshiriki na kunufaika kiuchumi, maendeleo na ustawi wao.

# KONGAMANOLAUWEKEZAJILILIVYOTANGAZAZATANGA

**Na Emma Kigombe, OMM TANGA**




*Waziri wa Ncho Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Mhe Prof Kitila Mkumbo, akifungua Kongamano la Uwekezaji akihutubia kwenye Kongamano la Kutangaza na Kuzindua Mwongozo wa Uwekezaji, Biashara na Utalii mkoani humo.*

Kongamano la Kutangaza na Kuzindua Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji, Biashara na Utalii mkoani Tanga, lililofanyika Novemba 15 hadi 17, mwaka jana, lilikuwa lenye ufanisi mkubwa, likiwashirikisha wadau kutoka sehemu tofauti za ndani na nje ya nchi.

Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa, akiwakilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na uwekezaji ), Mhe Profesa Kitila Mkumbo, alifungua kongamano hilo, na kuzindua Mwongozo wenye kuainisha fursa za uwekezaji, biashara na utalii zilizopo mkoani Tanga.

Miongoni mwa washiriki wa kongamano hilo la pili mkoani Tanga, baada ya jingine lililofanyika miaka 10 iliyopita walikuwa wawekezaji wa ndani na wale wa nje na mabalozi wa Tanzania waliopo nchi tofauti duniani, walioshiriki pia kwa njia ya mtandao.

Wengine ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, waliowahi kuwa Wakuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Martine Shigila (ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Geita), Adam Malima (Mkuu wa Mkoa wa Morogoro), Mhe Waziri Kindamba (DART), Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Mhe Profesa Mkumbo akasema Mwongozo uliozinduliwa utahamasisha zaidi uwekezaji wa ki-mkakati utakaochochea maendeleo ya uchumi na kuweka msisitizo katika uwekezaji endelevu unaowajibika kwa mazingira na manufaa kwa jamii.

Mhe Profesa Mkumbo alisema, Mwongozo huo umeeleza kwa kina fursa za kiuchumi zinazopatikana mkoani Tanga na ambazo zinaendana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan, katika masuala ya biashara na uwekezaji, lengo likiwa ni 'kuifungua nchi' kwa kuwakaribisha wawekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya kisekta nchini.

"Falsafa inayomwongoza Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan katika masuala ya biashara na uwekezaji ni kufungua nchi, fedha hazitengenezwi na Serikali bali zinatengenezwa na wawekezaji, '' alisema.

Aliongeza, ''kwa hiyo kazi ya Serikali tuliyoahidi ni kuweka mazingira rafiki na mazuri, ili watu wafanye biashara itakayotengeneza ajira na watu wapate kipato kupitia ajira hizo."

Mhe Profesa Mkumbo alisema, umuhimu wa sekta binafsi unatokana na mchango wake katika kutengeneza ajira ambapo takwimu zinaonyesha kuwa ajira 95 kati ya 100 zilizopo nchini,zinatengenezwa na sekta binafsi, wakati tano pekee zinatoka serikalini na taasisi za umma.

Mhe Profesa Mkumbo akaelekeza mamlaka zinazohusika kwenye mchakato wa uwekezaji nchini, kuondoa urasimu usio wa lazima kiasi cha kuwakatisha tamaa wawekezaji wenye nia thabiti ya kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Pia, Mhe Profesa Mkumbo akaziagiza mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji, na kuyawekea miundombinu muhimu ikiwemo barabara, maji na umeme.

Kwa upande wa fursa za uchumi wa buluu, Mhe Profesa Mkumbo aliutaka mkoa wa Tanga usimamie suala la uvunaji endelevu wa mazao ya bahari, ili kila raia anufaike na rasilimali hizo.

"Tanga ina kila aina ya samaki, jielekezeni kufanya uvuvi endelevu na kuongeza thamani ya mazao ya bahari, ili kila mmoja anufaike na uwepo wa bahari na mazao yake," alisema Mhe Profesa Mkumbo.

# SAMIA ALIVYOIVUSHA BUMBULI KUTOKA HOSPITALI, NYUMBA ZA WATUMISHI HADI KUMILIKI JENGO




*Jengo jipya la halmashauri ya wilaya ya Bumbuli mkoani Tanga.*

**Na Vumilia Ngajua, BUMBULI**

Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli imetokana na halmashauri ya wilaya ya Lushoto Mwaka 2012, kama ilivyotangazwa katika Gazeti la Serikali na kuanza rasmi Februari 2013.

Hiyo ilikuwa ni baada ya kumegwa eneo la jimbo la Bumbuli. Halmashauri hiyo ina tarafa tatu za Soni, Mgwashi na Bumbuli, kata 18, vijiji 83 na vitongoji 673.

Halmashauri ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 700.8 na sehemu kubwa yake ni imezungukwa na safu za milima ya Usambara, mito na mabonde.

Shughuli kuu za kiuchumi za wananchi wa Bumbuli ni kilimo na ufugaji, zao kuu la biashara ni chai.

Mazao mengine ni ndizi, kahawa, katani, viungo, miwa na parachichi. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Bumbuli ilikuwa na watu 159,373.

Kutokana na halmashauri hiyo kuwa changa, ililazimika kutumia majengo ya hospitali ya kanisa la Lutheran yaliyokuwa kijiji cha Mission, kata ya Bumbuli kuanzia mwaka 2013 hadi 2015.

Mwaka 2015, halmashauri ilihamia katika nyumba za watumishi zilizopo kitongoji cha Ugunga, kata ya Bumbuli hadi Julai, 2023 ilipohamia Kwehangala.

Kwa kupitia Serikali ya Mhe Dk Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bumbuli ilipokea fedha kwa awamu hadi kufikia Shilingi bilioni 5.6 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya ujenzi wa jengo lake. Ujenzi huo ulianza 2018/2019.

Julai, 2023 Halmashauri ilihamia kwenye jengo jipya lililopo kitongoji cha Dai, kijiji cha Kwehangala ambapo gharama zake hadi kukamilika ni Shilingi bilioni 6.1.

Jengo hilo la ghorofa mbili, lina vyumba vya ofisi 72, vinavyotumiwa na wakuu wa idara, vitengo, wasaidizi, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwenyekiti wa Halmashauri, kumbi za za vikao na masijala.

Pia kuna vyumba vya mifumo, mghahawa, chumba maalumu cha kuhifadhia mitihani, matenki manne ya kuhifadhia maji, tanki la chini ya ardhi lenye ujazo wa lita 75,000 na matanki matatu ya juu yenye ujazo wa lita 15,000 kila moja, mifumo ya ulinzi na usalama wa jengo.

Jengo hilo limezingatia mahitaji ya watu maalimu ikiwemo sehemu za kupita watu wenye ulemavu.

Uwepo wa ofisi hiyo umesaidia kurahisisha utendaji kazi wa watumishi na kutoa huduma bora kwa wakati, ambapo hapo awali iliwawia vigumu watumishi kutoa huduma bora.

Hivyo, manufaa ya jengo hilo yanajumuisha uwepo wa mazingira bora ya utendaji kazi, ongezeko la motisha, ufanisi wa utendaji kazi, huduma kwa wananchi imesogezwa ambapo kabla, wananchi walilazimika kwenye Lushoto kupata huduma.

Nyingine ni kupunguza umbali na gharama kwa wananchi kupata huduma, kuboresha huduma za kisekta kama vile kilimo, mifugo, elimu, afya, usimamizi wa miradi ya maendeleo, misitu, mazingira na utawala.



*Sehemu ya majengo ya zilizokuwa ofisi za zamani za halmashauri ya wilaya ya Bumbuli.*

# NHC KUTUMIA BILIONI 1.7 UJENZI WA NYUMBA TANGA




*Mfano wa nyumba ya NHC itakayojengwa Mkwakwani mkoani Tanga.*

**Na Mashaka Mgeta, OMM TANGA**

Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linaendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka 10, miongoni mwa malengo msingi ni ujenzi wa nyumba 300,000 kwa matumizi ya makazi, ofisi na biashara.

Mkakati huo ulioanza kutekelezwa 2015 na kufikia ukomo wake mwaka huu, unahusisha ujenzi wa nyumba hizo kwenye maeneo ya kimkakati kibiashara, mahali palipo na mahitaji makubwa kwa matumizi yake.

Meneja wa NHC Mkoa wa Tanga, Mhandisi Mussa Kamendu, amesema Tanga ni miongoni mwa mikoa inayoguswa na utekelezaji wa mkakati huo ambapo, kwenye mtaa wa Mkwakwani, kunajengwa nyumba kwa matumizi hayo tofauti ya biashara, ofisi na makazi.

Mhandisi Kamendu amesema, ujenzi huo utakaogharimu Shilingi bilioni 1.7 utaanza kutekelezwa Machi 10, 2025 na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja.

Kwa mujibu wa Mhandisi Kamendu, malengo ya shirika hilo ni kujenga nyumba zilizo kwenye mfumo wa kuhimili matumizi tofauti, huku zikiongeza thamani ya ardhi na hadhi ya mahali pa ujenzi, na mapato kwa shirika hilo.



*Mfano wa nyumba ya NHC itakayojengwa Mkwakwani mkoani Tanga.*

# MAPANGO YA AMBONI: URITHI WA ASILI ULIOJAA



*Sehemu ya Mapango ya Amboni mkoani Tanga.*

**Na Mwandishi wetu, NCAA.**

Jiji la Tanga lililopo kaskazini mashariki mwa Tanzania, lina historia kubwa katika pwani ya Afrika Mashariki. Tanga inajivunia kuwa mwenyeji wa moja ya maajabu ya kiasili na historia, yanayojulikana kama Mapango ya Amboni.

Mapango haya yapo umbali wa takribani kilomita tisa kutoka katikati ya jiji la Tanga, na yamejaa siri za zamani na za kipekee, zenye urithi wa kijiografia na hadithi zinazovutia kuhusu chimbuko lake katika historia ya Tanzania.

**ASILI YA JINA “AMBONI”**

Kwa mujibu wa simulizi za wakazi wa eneo linalozunguka mapango hayo, jina “Amboni” lina uhusiano wa moja kwa moja na Mama Mboni, mkazi wa eneo hilo aliyekuwa na shamba kubwa, akilima mazao mbalimbali.

Wakati wa ukoloni, wazungu walipendezwa na eneo hilo na walitaka kujenga kiwanda, huku wakimteua Mama Mboni kuwa msimamizi mkuu.

Kutokana na ugumu wa kutamka jina lake, wakoloni walilitamka vibaya na badala ya “Mboni,” wakaita “Amboni”, jina ambalo lilibaki na kuzoeleka hadi leo.

Mwaka 1892, kampuni ya Amboni Limited iliyokuwa ikimiliki mashamba ya Mkonge katika mkoa wa Tanga, ilimiliki eneo hilo la mapango na kuanza kulitumia kama sehemu ya kupumzikia.

Chimbuko la mapango hayo ni mabadiliko ya nguvu za asili, zilizobadilisha maumbile ya miamba ya chokaa kipindi cha Jurasiki (Jurassic period) miaka milioni 150 iliyopita.

Kulingana na utafiti uliofanywa, eneo hilo la Mapango lilikuwa chini ya maji miaka milioni 20 iliyopita, na linakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 234, lenye mazingira ya uoto wa asili.

Serikali ya Tanzania ilianza kutangaza eneo la mapango hayo kuwa eneo la hifadhi mwaka 1922, mwaka 1937 Serikali ilipitisha Sheria ya Mambo ya Kale iliyofuatiwa na ile ya mwaka 1953, ambayo imesaidia kulinda mambo ya kale.

**URITHI WA KIJIOGRAFIA NA KIHISTORIA.**

Mapango ya Amboni yenye umri wa zaidi ya miaka milioni 150 iliyopita na kuaminika kuwa yalikuwa sehemu ya bahari katika enzi hizo za kale, maji ya bahari yalichonga mawe ya chokaa na kuunda mandhari ya kuvutia ya mawe yaliyokolea michoro ya asili na miundo ya kushangaza.

Mwaka 1954, Mapango ya Amboni

# HISTORIA YENYE SIRI ZA MAMILIONI YA MIAKA

yalitangazwa kuwa sehemu ya urithi wa kitaifa, chini ya utawala wa kikoloni.

Baada ya uhuru wa Tanganyika, mapango yalihifadhiwa chini ya wizara mbalimbali, hatimaye mwaka 2019 yakakabidhiwa rasmi kwa usimamizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi, kuyalinda, kuboresha miundombinu na kuyatangaza ili kuendelea kuvutia wageni wengi kiutalii.

**AMBONI NA UHURU WA TANGANYIKA**

Katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika, wapigania uhuru walitumia mapango haya kama maficho yao dhidi ya wakoloni.

Njia za ndani ya Mapango ya Amboni zina maunganisho mengi ya asili, yaliyowaruhusu kujificha na kupanga mikakati yao bila kugundulika kwa urahisi na maadui ama wapinzani.

Aidha, kwa jamii za wenyeji wa Tanga walio jirani na mapango hayo zikijumuisha makabila ya Wadigo, Wasambaa, Wabondei na Wasegeju, waliyatumia kwa matambiko ya mizimu tangu Karne ya 16, na kufanya shughuli za kitamaduni.

Mpaka sasa, baadhi ya sehemu za mapango haya zinatumika kwa shughuli za matambiko, ambapo wenyeji huomba mvua, baraka na ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kijamii.

**UTALII**

Kwa sasa, kati ya mapango saba yanayohifadhiwa, matatu yanatumika kwa shughuli za utalii. Mawili kati ya hayo yanatumika kwa utalii wa kihistoria na maumbile, huku moja likitumika kwa shughuli za kitamaduni kwa wenyeji wa maeneo hayo.

Watalii wanaotembelea Mapango ya Amboni wanapata fursa mbalimbali ikiwemo maelezo ya kina kuhusu historia ya mapango na hadithi zake za kuvutia, kushuhudia maumbo ya ajabu ya mawe yaliyoundwa na mabadiliko ya kijiografia kwa mamilioni ya miaka.

Pia watalii wanapata uzoefu wa mandhari ya kipekee yenye mwanga hafifu, wa asili unaotengeneza mandhari ya kichawi na watalii kujifunza jinsi mapango haya yalivyohifadhiwa na mchango wake katika uhuru wa Tanzania.

Kwa mujibu wa takwimu za NCAA, zaidi ya watalii 30,000 wa ndani na wa kimataifa hutembelea mapango hayo kila mwaka, wakivutiwa na historia, simulizi, mazingira asilia na ya kuvutia na urithi wa utamaduni.

Mapango ya Amboni siyo tu kivutio cha utalii, bali pia ni hazina ya historia, utamaduni, na jiografia ya Tanzania. Kwa yeyote anayetamani kushuhudia maajabu ya maumbile, kufuatilia historia ya mapambano ya uhuru, au kushiriki katika mila na desturi za wenyeji na ni sehemu inayostahili kutembelewa.

**Karibu Tanga kutembelea katika Mapango ya Amboni sehemu ambapo historia, asili, na utalii hukutana!**



*Sehemu ya Mapango ya Amboni mkoani Tanga.*

# LUSHOTO TUNAKIRI, 'MAWE' YA MAMA SAMIA TUNAYAONA




*Jengo la Mama na Mtoto.*

**Na Selemani Shineni, LUSHOTO**

Jamii zina misemo mingi yenye kutafakarisha na kutoa tafsiri tofauti, kadri ya kusudio husika. Kwenye makala haya, nitatumia misemo kadhaa inayotoa inayoakisi mafanikio ya utawala wa Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan katika halmashauri ya wilaya ya Lushoto mkoani Tanga.

Kwanza, Wasambaa wanasema, 'nguvu ya mazi ni mawe', ikimaanisha 'nguvu ya maji ni mawe'. Waingereza wana msemo wao, 'actions speaks louder than words' kwa tafsiri isiyo rasmi kuwa, vitendo ni muhimu zaidi kuliko maneno na Waswahili wanasema, 'kuona ni kuamini' wakati vijana mitaani wanauliza, 'kusoma huwezi, hata picha huoni?'

Tuanze na Wasambaa wanaposema 'nguvu ya maji ni mawe' walimaanisha maji mengi na yenye nguvu yakipita sehemu, mawe yaliyopo kwenye njia ama mkondo wa maji yanatumika kama ushahidi wa kuwa maji yaliyopita sehemu hiyo, yalikuwa na nguvu kiasi gani.

Kwa halmashauri ya wilaya ya Lushoto, unapoizungumzia miaka minne ya Mhe Rais Dk Samia madarakani, ni kama maji yenye nguvu yaliyoacha mawe yamesimama kama ushahidi.

Kwa mukhtadha huo, maji yanakuwa kiwakilishi cha kazi kubwa anazozifanya Mhe Rais Dk Samia kuwatumikia wananchi, wakati matokeo yanayohusisha miradi mikubwa na huduma bora kwa jamii, vinawakilishwa na mawe yanayoonekana.

Mawe hayo ndio miundombinu inayojengwa katika sekta mbalimbali kama elimu, kilimo, mifugo, afya, barabara, nishati, utalii, demokrasia, usawa, haki, usafiri na usafirishaji na kadhalika.

Vitendo ni muhimu kuliko maneno, hili linathibitika katika utawala wake unaoghubikwa na maneno machache, lakini vitendo kwa maana ya kazi, zinazonekana kwa wingi na kuwanufaisha Watanzania.

Inawezekana wapo wasioamini hadi waone. Yapo mengi yanayoonekana. Na kwa wasiojua kusoma wakatakiwa kuona hata picha, hiyo ni kwa maana ya uhalisia wa vitu na huduma za maendeleo na ustawi kwa wananchi vinavyopatikana katika utawala wa Mhe Rais Dk Samia.

Mafanikio hayo ndiyo fahari ya wakazi wa halmashauri ya wilaya ya Lushoto, kwa kuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa.

Mathalani, katika kipindi cha

*Inaendelea uk 33*

*Inatoka uk 32*

miaka minne hiyo, umeme umefika kwenye kata zote 33, vijiji vyote 125 na vitongoji tisa vya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lushoto vimefikiwa na umeme.

Upande wa barabara ilikuwa moja ya kuingia halmashauri hiyo, yaani Lushoto – Soni – Mombo, lakini sasa zipo barabara nyingine za Hekcho hadi Mkomazi, Mtae hadi Mnazi na Ngulwi hadi Mombo.

Katika sekta ya maji, tarafa zote tano za halmashauri hiyo kuna miradi mikubwa ya maji inayotekelezwa au imetekelezwa, ikiwa na lengo la kutimiza azma ya Mhe Rais Dk Samia kumtua Mama ndoo kichwani. Sehemu ya miradi hiyo ni ile iliyopo Magamba na kwenye kijiji cha Tewe.

Kwenye elimu yapo mengi, lakini kwa uwakilishi, watoto wa Lushoto ni miongoni mwa wanaonufaika na kusoma kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita bure, na wana uhakika wa kupata mkopo wa elimu ya vyuo vya kati na vikuu.

Ieleweke kuwa, kabla ya Mhe Rais Dk Samia kuingia madarakani, halmashauri ya wilaya ya Lushoto ilikuwa na shule 51 za sekondari, zimeongezeka kufikia 60.

Katika sekta za kilimo na mifugo, Lushoto imetoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima, pikipiki 35 na vishkwambi 42 kwa maafisa ugani.

Pia kumefanyika ukarabati wa skimu za umwagiliaji Mng'aro, ujenzi wa mnada wa mifugo Lunguza, ujenzi wa kituo cha kukusanya maziwa na usambazaji wa madume bora 20 ya mbegu kwa wafugaji katika tarafa ya Umba.

Kwa upande wa afya, Lushoto imepokea zaidi ya Shilingi milioni 807.55 za ukarabati wa hospitali ya wilaya ya Lushoto.

Pia, vituo vya afya vimeongezeka kutoka vinne hadi nane, zahanati kutoka 46 hadi 66, ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya, magari manne ya kubeba wagonjwa na akina mama 231 na watoto wachanga 34 wanufaika kwa huduma za m-mama.

Lushoto imenufaika kwa ukamilishwaji wa jengo la Mama na Mtoto, na ununuzi wa vifaa tiba vilivyogharimu zaidi ya Shilingi milioni 929.4.

Kwa haya machache, halmashauri ya Lushoto chini usimamizi wa Mkuu wa Wilaya, Mhe Zephania Sumaye, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe Mathew Mbaruku na Mkurugenzi Mtendaji, Dk Ikupa Mwasyoge, 'mawe' yameonekana kuashiria nguvu ya maji. Ndiyo matokeo ya kazi na utumishi wa Mhe Rais Dk Samia kwa Watanzania.



*Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Mhe Zephania Sumaye.*

# UTALII WA MAJINI UNAYOWEZA KUKUFIKISHA KISIWA CHA TOTEN



**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

Toten ni kisiwa kinachopatikana kwenye hori ya Tanga katika bahari ya Hindi. Jina la kisiwa hiki chenye mvuto wa kipekee, linatokana na lugha ya Kijerumani 'Toteninsel' ikimaanisha "Kisiwa cha Wafu."

Simulizi za kimapokeo zinaeleza kuwa, Wajerumani walitumia jina hili walipoifanya Tanga kuwa bandari muhimu ya koloni lao katika ukanda wa Afrika Mashariki, kwa sababu kulikuwa na makaburi mengi kisiwani humo.

Waingereza walipochukua utawala kutoka kwa Wajerumani, walikiita kisiwa hicho "Toten Island" wakichukua "Toten" kama jina ambalo hawakutafsiri maana yake.

Kisiwa hicho kina eneo la takriban hekta 16. Umbile lake linaaminika kuwa na umbo la tanga la kwenye jahazi.

Ndani ya kisiwa hicho kuna magofu ya msikiti wa karne ya 17, na makaburi ya karne ya 18 na 19.

Pia, kuna vipande vya vyungu vinayopatikana ndani ya kisiwa hicho, ambavyo ni dalili ya kwamba kilikaliwa na watu walioondoka baadaye.

Inaelezwa kuwa, kisiwa hicho ambacho kipo umbali mchache kutoka bandari ya Tanga, pia kilitumika kuwatenga watu waliokuwa na magonjwa ya hatari kama vile ukoma.

Kwa sasa kisiwa hicho kinatumika kwa kazi ya kutembeza watalii ambao husafirishwa kwa boti na ngarawa kutoka pwani ya Tanga hadi katika eneo hilo, kwa ajili ya kujionea mambo mbalimbali ya kihistoria yaliyomo.

## BUSTANI YA JAMHURI

NI mahali penye mandhari ya kuvutia kwa mapumziko ya mtu mmoja, kikundi ama jumuiya ya watu, ikipata upepo mwanana kutoka bahari ya Hindi.

Mahali hapo ni bustani ya Jamhuri maarufu kama Forodhani, iliyo maridhawa, pembeni mwa ufukwe wa bahari jijini Tanga.

Ukiwa unabarizi kwenye bustani hiyo inayonakshiwa kwa kiingereza kama Jamhuri Park, pembeni yake kuna maktaba ya mkoa wa Tanga.

Pia ni mahali unapoiona vizuri mandhari ya kisiwa cha Toten na bandari ya Tanga.
Miundombinu ya bustani hiyo inajumuisha maeneo mahususi ya kuketi kwa ajili ya watu kupumzika na kupunga upepo, mahali ambapo watu wanaweza kunong'onezana pasipo walio jirani yao kusikia, ama wakaongeza sauti kadri wanavyotaka.

Bustani hiyo ni miongoni mwa miradi ya halmashauri ya jiji la

***Inaendelea uk 35***

*Inatoka uk 32*
Tanga, ukiwa umeboreshwa kwa gharama za Shilingi bilioni mbili za ufadhili wa taasisi ya Botnar Fondation.

Lengo la mradi huo ni kuboresha sehemu za mapumziko kwa familia, na kuwa sehemu inayotoa fursa ya biashara zinazowapatia kipato wakazi wa Tanga, hivyo kujikimu kimaisha.

Kwenye bustani hiyo kuna huduma mbalimbali kama za vyakula, vinywaji na michezo ya watoto.

## MAGOFU YA TONGONI NA ZIARA YA VASCO DA GAMA



Ni magofu ya waswahili yaliyorekodiwa karne ya 15. Magofu hayo ya msikiti na makaburi arobaini yapo katika kata ya Tongoni wilaya ya Tanga.

Tofauti na mwonekano wake wa sasa, simulizi zinaeleza kuwa Tongoni ulikuwa mji na kitovu cha biashara cha waswahili, uliostawi na kuheshimiwa sana katika karne ya 15.

Mji mkongwe wa Tongoni ulianzishwa na waswahili karibu na karne ya 11, kama sehemu ya majimbo ya miji mbalimbali ya uswahilini iliyo kando ya pwani ya Afrika Mashariki.
Vasco da Gama, baharia wa Ureno, alitembelea mji wa Tongoni kwa mara ya kwanza Aprili 1498.

Alipata fursa ya kula machungwa ya kienyeji kwenye mji huo, ambayo alisema ni bora kuliko yale yanayopatikana kwao Ureno.

Alifanya ziara ya pili mwaka uliofuata, yaani 1499 na alikaa siku 15 mjini Tongoni. Magofu ya mji wa kale wa Tongoni yako chini ya Idara ya Mambo ya Kale Tanzania iliyopo kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Yapo wazi kwa umma.

## UWEKEZAJI WA KITALII

Uwekezaji kwenye maeneo ya sekta ya utalii unajumuisha ujenzi wa miundombinu ya kusaidia utalii kama hoteli zilizopo kwenye fukwe za bahari ya Hindi kama vile Chongoleani, Mwambani, Tongoni na Mwarongo.

Pia, kwenye fukwe za Tanga kuna utalii wa kuendesha mashua za mashindano ya baharini, kuogelea kwa kupiga mbizi, utalii wa utamaduni wa wenyeji wa Tanga na mwenendo wa maisha yao kwa jumla.

## PANGANI NA WINGI WA VIVUTIO VYA UTALII TANGA

PANGANI ni mji uliopo ufukweni mwa bahari ya Hindi kati ya Dar es Salaam na Tanga. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Pangani ina watu 75,642.

Mji huo una historia ndefu, hasa kwa sababu kuna bandari nzuri ya asili inayofaa kwa majahazi madogo.

Majengo mbalimbali ya kale ni ishara ya historia ndefu ya mji huo. Historia hiyo inapambwa na boma lililojengwa na waarabu wa Unguja na kutumiwa na wakoloni wa kijerumani na kiingereza, na pia kuna nyumba za waswahili.

Eneo la mji limegawinywa katika kata mbili ambazo ni, Pangani Mashariki (pamoja na mji wa kihistoria) na Pangani Magharibi.

Mji wa Pangani upo kando ya hori ya bahari ya Hindi, mahali ambapo Mto Pangani unaishia. Hori ina upana wa kilomita tano, ikiingia nchi kavu umbali wa kilomita mbili na nusu.

Mdomo wa mto Pangani una upana wa mita 300 - 500 kilomita kadhaa ndani ya nchi kavu, na hivyo ni bandari salama kwa jahazi ndogo.

Mji wa Pangani ulianzishwa upande wa Kaskazini wa mdomo wa mto Pangani kwenye pwani, katikati ya visiwa vya Unguja na Pemba. Bandari ya Pangani inafikiwa na jahazi ndogo.

Ndani ya mdomo wa mto Pangani, merikebu zilikuwa salama hata wakati wa dhoruba baharini.

Uzuri wa bandari hiyo ulikuwa msingi wa kustawi kwa mji kama kituo cha safari kwenye pwani na mahali pa biashara kati ya bara na visiwa vya Unguja na Pemba.

Sehemu ya bahari ya Hindi kwenye pwani ya wilaya ya Pangani na maeneo ya fukwe na ukanda huo, yanaweza kupanua wigo wa biashara ya utalii wenye kuhusisha utamaduni na mazingira, kwa kupumzika ufukweni, kucheza michezo mbalimbali ya baharini kama kupiga mbizi.

Pia kuna kuzamia, kuogelea, uvuvi wa mashindano, kulala mchangani, mashindano ya mbio za ngarawa na mashua, kupiga picha na kufanya pikiniki kutokana na kuwa na fukwe nzuri zenye mchanga msafi usio na tope.

Maeneo hayo yanawezesha watalii kutembea masafa mafupi na marefu, kubarizi upepo mwanana, uvuvi wa kienyeji kwa

• ***Inaendelea Uk 36***

• *Inatoka Uk 35*

ngarawa na uvuvi wa kibiashara ili kutosheleza soko la ndani na nje, kilimo cha mwani na hoteli nyingi zinazohitaji samaki wa kutosha kwa ajili ya watalii wanaofika Pangani.

Kwa kuwatumia waongoza watalii wenye ujuzi na kazi hiyo kutoka kwenye Kituo cha Utalii Pangani, watalii wa nje na ndani ya nchi huoneshwa maeneo ya kihistoria ya mji mkongwe wa Pangani na ukuta wa bahari.

Pia kuna minara ya makumbusho, majengo ya kihistoria ujenzi wa mawe na chokaa yenye nakshi na milango ya kuvutia, misikiti, uwanja wa Uhuru, magofu na makaburi ya chimbuko la mji wa Pangani ya Mhembo, Kumba, Bweni na miji mingine maarufu ya kale ya Ushongo, Kipumbwi, Mkwaja na Buyuni.

### HAUJAWAONA KASA WA KIJANI? NENDA KISIWA CHA HIFADHI YA MAZIWE



KISIWA cha hifadhi ya Maziwe ni maarufu kwa utalii wa kuangalia kasa wa kijani wanapokwenda kutaga.

Kisiwa hicho ni maarufu pia kwa michezo ya kupiga mbizi, kuogelea, kupiga picha, kulalamchangani, kuona nguva na kuona samaki wa aina mbalimbali.

Utalii kwenye kisiwa hicho unakuwezesha kuona maisha na ekologia ya bahari, matumbawe na kufanya utafiti.

Usafirishaji wa watalii kwenda kisiwani unaongeza pato la Serikali na uchumi wa wananch.

### MTO PANGANI



MTO huu maarufu maji yake yanatokea mlima mrefu barani Afrika wa Kilimanjaro.

Ni mto pekee wenye maji safi unaoingiza maji yake kwenye bahari ya Hindi.

Watalii wanapenda kusafirishwa katika mto huu kwa kutumia mashua, ili kuona uoto wa mikoko, ndege wa aina mbalimbali, wanyama wadogo kama kima, tumbili, mbega na wanyama wakubwa kama mamba, viboko, samaki, kamba na ufugaji wa kaa kwenye mikoko ambayo ina ikolojia ya pekee ya mazalia ya viumbe hao na uvuvi wa asili.

Mto Pangani pia ni chanzo cha umeme wa maji katika mji wa Hale, wilaya ya Korogwe.

### HIFADHI YA TAIFA YA SAADANI

HIFADHI ya Taifa Saadani ni miongoni mwa vivutio vya utalii mkoani Tanga.

Hifadhi hiyo ipo Kusini mwa mkoa wa Tanga, unapopakana na wilaya ya Bagamoyo na makao yake makuu yako katika wilaya ya Pangani maeneo ya Mkwaja.

Hifadhi ya Saadani ina miti mingi ya miombo, migungana na mikoko inayoota kwenye mito inayoingia bahari ya Hindi. Watalii wakifika kwenye hifadhi hii wanapokewa na waongozaji watalii wenye ujuzi na weledi na kuna hoteli za kuvutia kando na ndani ya hifadhi.

Wanyama wa aina mbalimbali kama simba, tembo, chui, nyani, punda milia, nyati, nyoka, vipepeo, nyuki na ndege wa aina mbalimbali wanapatikana ndani ya hifadhi hiyo.

Kwenye hifadhi hiyo, watalii wanaifurahia kuona maisha ya viumbe wa baharini na mbuga za wanyama, wakiwemo kasa wa kijani kwenye mazalia ya kasa Madete.

### HIFADHI YA MSITU WA AMANI

HIFADHI ya Msitu wa Amani iliorodheshwa rasmi mwaka 1997 kwa ajili ya kulinda wanyama na uoto wa flora na fau.

Katika hifadhi hiyo, upande wa Mashariki na Magharibi ni milima ya Usambara ambayo ni sehemu muhimu kwa viumbe hai.

Hifadhi ya Msitu Amani inajumuisha makazi ya misitu ya tropiki yenye mawingu. Hifadhi hiyo imekuwa kivutio kizuri cha utalii, kwani imezidi kukua na kuongezeka.

Eneo hili la hifadhi lililopo katika wilaya za Muheza na Korogwe mkoa wa Tanga, lina makundi makubwa ya ndege, vipepeo na miti ambayo mingine hupatikana katika hifadhi hii tu.

Pia kuna nyani weupe, weusi na wa rangi ya buluu.

• *Inaendelea Uk 37*

• *Inatoka Uk 36*

Kwenye hifadhi hii kuna aina tisa za mimea jamii ya violeti na ndege kama bundi na tai aina ya Nduk Eagle owl wanaopatikana katika hifadhi hiyo pekee.



**MSITU WA MAGOROTO**

MAGOROTO ni msitu maarufu wa kitropiki unaopatikana kwenye wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Awali, msitu huo ulikuwa mashamba ya watawala wa kijerumani na baadaye ukahifadhiwa kama sehemu muhimu yenye uoto wa asili.
Upekee wake ni kuwapo kwa ziwa lililotengenezwa na binadamu lenye viumbe hai mbalimbali, wakiwamo samaki.

Msitu huu wenye ukubwa wa ekari 591 na ziwa la maji safi, ulifunguliwa mwaka 1896 na watawala wa kijerumani kama shamba la kwanza la kibiashara Afrika Mashariki.
Kwa mara ya kwanza, shamba hilo lililimwa zao la mpira baada ya kushindwa kulima kahawa na chai, na baadaye kulimwa michikichi mwaka 1921.

Eneo hilo lilichukuliwa na wazawa 'kundi la Amboni' mwaka 1940 na kilimo cha michikichi kilisitishwa baada ya kuwapo ushindani kutoka Malaysia na Indonesia.

Baada ya hapo, msitu wa Magoroto ulihifadhiwa mpaka leo kwa kuzingatia upekee na uzuri wake.

Pamoja na kupakana na msitu wa Mlinga, Magoroto inatengeneza 'vipande' vya milima ya Usambara ambayo inafahamika kwa uzuri na upekee wa uoto wa asili.

Msitu wa Magoroto unafahamika zaidi kwa uwapo wa ndege wa pekee, ambapo Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) na Chama cha Uhifadhi Wanyamapori wamechukua jukumu la uhifadhi wa misitu hiyo nchini.

**SAFU YA MILIMA YA USAMBARA**



MILIMA ya Usambara ni sehemu iliyoinuka upande wa kaskazini mashariki mwa Tanzania.

Ni milima kunjamano, yaani milima iliyoshikana kutoka mlima mmoja mpaka mwingine.

Wenyeji wanaoishi maeneo hayo ni wasambaa. Safu ya milima hiyo imeenea kuanzia wilayani Korogwe kuelekea kaskazini mpaka karibu na milima ya Upare.

Safu hiyo inajumuisha milima ya Bumba, Chambolo, Dindila, Gombelo, Gonja, Kagambe, Kilanga, Kilimandege, Kwagoroto, Kwashemhambu, Magamba, Makanja, Mashindei, Matundsi, Mavumbi, Mlomboza Myanko, Mzinga, Mzogoti, Nengoma, Shagein, Shemausha, Sungwi na Zumbu.

Milima ya Usambara ni sehemu ya milima ya Tao la Mashariki, ambayo inaanzia kusini mwa Kenya hadi kusini mwa Tanzania.

Miinuko hiyo ilitokea takribani miaka milioni 100 iliyopita, ikitengeneza milima na mabonde kwenye mstari wa zamani wa mabonde.

Milima hiyo inainuka juu ya tambarare zinazozunguka kama safu za pwani na hupata mvua za monsuni, zinazonyesha kwenye bahari ya Hindi.

**SAFU YA MILIMA YA USAMBARA**

HIFADHI ya Taifa ya Mkomazi ipo katika mikoa miwili ya Kilimanjaro na Tanga, ndani ya wilaya za Same na Lushoto.

Hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka 1951 kama Pori la Akiba, lililotengwa kutoka katika pori kubwa la akiba la Ruvu.

Ina ukubwa wa kilometa za mraba 3245 (kilometa za mraba 2010.4 ni Mkomazi na kilometa za mraba 1224.1 ni Umba).

Pori hili lilipendekezwa kuwa hifadhi ya taifa kwa misingi ya kunusuru maeneo na rasilimali zilizomo, kutokana na matumizi yasiyoendana na uhifadhi kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

Kwenye hifadhi hiyo, kuna wanyama na ndege wa aina mbalimbali wakiwamo mbwa pori na vifaru weusi walioingizwa kutoka Afrika Kusini.

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi iko Kaskazini mwa Tanzania, kati

• *Inaendelea Uk 38*

• *Inatoka Uk 37*

ya Moshi na Tanga. Ipo katika mazingira mazuri yenye milima ya Pare na Usambara juu ya mipaka yake.

Kulingana na hali ya hewa, Mlima Kilimanjaro unaweza pia kuonekana kutoka kwenye bustani.

Hifadhi hii ina zaidi ya kilomita za mraba 3,234 (hekta 323,400), na inatawaliwa na uoto wa Acacia- Commiphora; inapakana na mbuga ya taifa ya Tsavo Magharibi ya Kenya.

Eneo linalojulikana kwa jina la 'Mkomazi' ni muungano wa mapori mawili ya awali, pori la akiba la Umba upande wa Mashariki (wilaya ya Lushoto, mkoa wa Tanga) na pori la akiba la Mkomazi upande wa Magharibi (wilaya ya Same, mkoa wa Kilimanjaro).

Baadhi ya nhyaraka hifadhi hiyo inatajwa kama mapori ya akiba ya Mkomazi-Umba.

Kwa upande wa wanyamapori, Mkomazi ni hifadhi pekee Tanzania ambayo unaweza kuona aina adimu za Sahel Biosphere, ukanda wa nusu ukame unaonyoosha kusini kutoka Jangwa la Sahara.

Hizi ni pamoja na kudu kudu, gerenuk na beisa oryx.
Ardhi tambarare na pana ya Mkomazi, inazopakana na milima ya Pare na Usambara, hutoa fursa ya kutazama makundi makubwa ya wanyama kwenye mandhari ya kuvutia.

Pia Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ni kivutio kizuri kwa watazamaji wa ndege. Zaidi ya aina 450 za ndege zimerekodiwa, ikijumuisha ndege maalumu kama vile Shelley's starling na tchagra wenye milia.

Pia ni mahali pekee Tanzania ambako unaweza kuona ndege aina ya vulturine guineafowl. Ndege wakubwa wa ardhini kama mbuni, kori bustard, ndege katibu na pembe ya kusini ni kawaida sana kwenye nyanda za nyasi.

Aina ya ndege zinazohama kama vile roller za Ulaya zipo kuanzia Novemba hadi Aprili.
Historia ya hifadhi ya taifa ya Mkomazi, kama ilivyo kwa hifadhi nyingi za taifa na mapori ya akiba, ni ya mashindano, huku washindani wakuu wakiwa ni wapangaji wa uhifadhi wa serikali na watumiaji wa rasilimali za vijijini.

Mkomazi ilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, familia kadhaa za wafugaji kutoka kabila la Parakuyo ziliruhusiwa kuendelea kuishi humo na maelfu ya ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Serikali ya kikoloni ya wakati huo iliwaruhusu kuishi huko kwa sababu walikuwa wamekaa katika eneo hilo kwa miaka mingi, na walifikiriwa kutotishia uadilifu wa ikolojia ya hifadhi hiyo.




*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga, walipotembelea Hifadhi ya Mkomazi hivi karibuni*

# TAMASHA LA URITHI WETU 'LILIVYOITIKISA' TANGA




*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Dk Batilda Burian (katikati) akiwa jukwaani na baadhi ya akina mama walioshiriki Tamasha la Urithi hivi karibuni.*

**Na Mashaka Mgeta, OMM TANGA**

Tanga waja leo, kuondoka ni maajaliwa. Hiyo ni kauli inayobeba dhima yenye kutafsiri utamaduni msingi, unaofungamanishwa na mila na desturi za wakazi wa mkoa huo unaosifika kwa ustaarabu, ukiwa ni miongoni mwa maeneo yaliyopo kwenye ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi.

Makabila makubwa ni Wasambaa wanaopatikana zaidi kwenye maeneo yenye safu ya milimani ya Usambara katika wilaya za Muheza, Korogwe na Lushoto.

Wazigua waliopo zaidi kwenye wilaya ya Handeni na sehemu za wilaya za Korogwe na Pangani; huku Wabondei wakiwepo zaidi Muheza na sehemu za Pangani; na Wadigo wanaoaminika kuwa wengi kwenye jiji la Tanga na sehemu za wilaya ya Muheza.

Utamaduni wa Tanga unaoundwa na mambo kadha wa kadha yenye kunakishsha mahusiano ya watu, burudani na stadi za maisha, unajumuisha ujuzi wa mapishi ya vyakula vya asili na vile vya ubunifu wa kitamaduni.

Vyakula hiyo ni kama vile maharage ya kukata, ndizi za mkono wa tembo, yai la jicho la mke mwenza, chapatti za kurasa na chai ya kukaanga na zile zinazotengenezwa kwa nazi, pilipili na nanasi, manukato yenye harufu nzuri zinazofaa kwa matumizi tofauti ya binadamu kama vile mikutano na kwenye mapumziko na uturi yenye manukato.

Pia kuna michezo ya kama bao, kuruka kamba, mdako, na burudani za jadi ikiwemo Baikoko, Mdumange na Kijamvi.

Ili kutambua kuwa upo katika mkoa wa Tanga, haikwepeki kubaini aina ya mavazi yakiwamo ya vijora, viguberi, madera na baibui yanayotumiwa na wanawake na kanzu, baraghashia na msuli kwa wanaume.

Mambo hayo na mengine ambayo hayajatajwa kwenye makala haya, yanabeba maana halisi ya utamaduni wa Tanga na hivyo kuhitaji kutunzwa, kuendelezwa ili yarithishwe kwa kizazi hata kizazi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian, Desemba 24,2024 alitangaza kufanyika kwa Tamasha la Urithi Tanga, akishirikiana na wadau wengine, wakiwemo halmashauri za wilaya, miji na jiji, wajasiriamali na wawekezaji katika tasnia za utalii, biashara, uvumbuzi, wasanii na wabunifu.

Mhe Balozi Dk Batilda, alisema

***Inaendelea uk 40***

# TAMASHA LA URITHI WETU 'LILIVYOITIKISA' TANGA

*Inatoka uk 39*

lengo kuu ni kutunza na kutengeneza jamii inayochangamkia fursa za urithi wa utamaduni katika mandhari nzuri ya mkoa huo na ukanda wa pwani kwa ujumla.

Tamasha hilo likawaleta pamoja watu kutoka mikoa na nchi mbalimbali, wakiwakilisha nyanja zote za maisha, kusherehekea, kukuza urithi, kuheshimu mila, tamaduni , desturi na kukumbatia ubunifu na uzalendo uliopo nchini.

Mhe Balozi Dk Batilda akasema Tanga ni kitivo cha utamaduni na biashara, hivyo kuufanya mkoa huo kuwa mahali pazuri kwa tamasha hilo na mandhari yake ya kuvutia usanifu wa kihistoria na uwekezaji.

Mambo mengi mazuri yenye kuvutia, kuburudisha, kufundisha na kurithisha utamaduni wa Tanga yakafanyika wakati wote wa tamasha hilo ikiwemo ngoma za asili, maonesho ya vyakula vya asili ya Tanga, ziara za kihistoria, sanaa, ustaarabu wa pwani, uchumi wa buluu na kazi za ubunifu wa bidhaa zinazotengenezwa kwa kutumia katani na ukindu.

Tamasha hilo likahusisha pia burudani asilia na usiku wa khanga za kale, usiku wa alwatan, usiku wa mvuvi. Vyote hivyo vitapambwa na mavazi ya asili kama khanga za kale, baibui la ukaya, misuli na barakhashia.

### CHAI YA KUKAANGA

Aina ya chai zisizopatikana kwenye maeneo mengine ya nchi, ni miongoni mwa bidhaa zilizolifanya tamasha hilo kuwa la kipekee, na kuwaalika watu wengi zaidi kushiriki ili kuzishuhudia na kunywa chai hizo.

Zilikuwepo zinazotengenezwa kwa nazi, pilipili na chai ya kukaangwa.

Mamia ya wakazi wa jiji hilo wakiwemo wageni kutoka nje ya nchi, waliongozwa na Balozi wa Japan nchini, Yashushi Misawa, wakafika kwenye viwanja vya Kituo cha Urithi Wetu kushiriki tamasha hilo.

Wabobezi wa tasnia ya utamaduni, akiwemo mtafiti wa lugha, Njaidi Membe wakapata fursa ya kuwasilisha mada miongoni mwa hizo ikihusu Chimbuko la Makabila na Matumizi Sahihi ya Lugha ya Kiswahili

Kwenye orodha ya upekee wa Tanga, hauwezi kuacha kuyataja magofu na mitaa yake yenye namba kuanzia 1 hadi 21, iliyokuwepo tangu enzi za ukoloni. Mitaa hiyo na namba husika inaendelea kudumu hata sasa, ingawa haipewi kipaumbele kikubwa katika maelezo yanayobebwa na historia ya mali kale za mkoani humu.

Tamasha la Urithi wa Tanga likaibua asili na umuhimu wa mitaa hiyo, lakini kwa tahadhali kwamba, mitaa hiyo pekee, haiwezi kuwa kielelezo cha utitiri wa mambo ya kale yanayoashiria ama kuakisi utamaduni wa Tanga.



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi mkoa wa Tanga, walipotembelea Hifadhi ya Mkomazi*



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe Balozi Dk Batilda Burian (wa pili kulia), akizungumza na wageni kutoka nje ya nchi walioshiriki Tamasha la Urithi mkoani humo.*

# MRADI WA MIJI 28 UNAFUTA CHANGAMOTO ZA MAJI TANGA



*Ujenzi wa miundombinu ya kuchakata maji inayojengwa Mswaha Darajani, Korogwe ikiwa ni sehemu ya mradi wa Maji kwenye Miji 28 nchini.*

**Na Mwandishi Wetu, OMM TANGA**

MIAKA kadhaa iliyopita, viongozi wa Serikali walipoutembelea mkoa wa Tanga hasa kwa kutumia usafiri wa barabara, kisha kusimama Mkata katika wilaya ya Handeni, jambo lililotarajiwa kwa haraka ni kuwaona wananchi wameshika madumu, wakiashiria kuwepo kero ya maji mkoani humo.

Wakati huo, hali ya upatikanaji maji haikuwa ya uhakika kiasi cha kuwafanya wananchi hao kutembea umbali mrefu, wakitafuta rasilimali hiyo muhimu kwa maisha ya binadamu.

Hatua kwa hatua, Serikali ikabuni, kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ikiwemo uwekaji mtandao wa mambomba kutoka vyanzo tofauti vya uzalishaji maji, uchimbaji wa mabwawa makubwa ya kisasa, uboreshaji wa miundombinu chakavu ya usambazaji maji, miongoni mwa hatua nyinginezo nyingi.

Nia njema hiyo ya Serikali kwa wananchi wake imekwenda mbali zaidi kwa kuziunganisha wilaya za Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani kwenye mpango mkubwa ulio mahususi wa miji 28 nchini, kupata mradi wa maji safi na salama.

Kwa mkoa wa Tanga, mradi ulio chini ya Wizara ya Maji kupitia mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni (HTMWSSA) utagharimu Shilingi bilioni 171 zilizotolewa na Serikali ya India kama mkopo wa masharti nafuu .

Mkurugenzi Mtendaji wa HTMWSSA, Mhandisi Yohana Mgaza, alisema mradi huo wa miezi 32 unaotarajiwa kukamilika Desemba 10, 2025, unaohusisha kutoa maji Mto Pangani kwenda kwenye miji ya Handeni,

***Inaendelea uk 42***

*Inatoka uk 41*

Korogwe, Muheza na Pangani unatekelezwa na Mkandarasi M/s JWIL Infra Limited.

Mhandisi Mgaza alisema, mradi huo utaongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka mita za ujazo 5,500 hadi 52,000 kwa siku na utatimiza mahitaji ya maji kwa miaka 20 ijayo.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mgaza, kazi zilizopangwa kufanyika kwenye mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio lenye ukubwa wa lita milioni 52 kwa siku, kutoka katika chanzo cha mto Pangani kwenye kijiji cha Mswaha Darajani.

Nyingine ni chujio lenye ukubwa wa lita milioni 51 kwa siku, nyumba za watumishi eneo la chujio, ofisi, vituo viwili vya kusukumia maji kwenye kata za Kwamatuku na Sindeni wilayani Handeni.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mgaza, kazi nyingine ni ulazaji wa bomba kuu la maji lenye kipenyo kati ya milimita 150 hadi 800 na urefu wa kilomita 188 kutoka Handeni hadi Pangani.

Pia kuna matenki nane ya kuhifadhi maji yenye ukubwa tofauti kuanzia lita 200,000 hadi 2,000,000 kwenye maeneo ya Vibaoni, Bongi na Segera (Handeni), Kwafungo na Kilulu (Muheza), Ubanga, Madanga na Boza (Pangani)



*Tenki la kuhifadhi maji lililopo eneo la Vibaoni wilayani Handeni.*

# TANGA: MKOA WENYE FURSA NYINGI ZA UWEKEZAJI



*Mchimbaji mdogo wa madini kwenye mgodi wa Kwandege wilayani Handeni, Godfrey Bitesigirwe (aliyenyoosha mkono) akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe Albert Msando (wa kwanza kulia).*

**Na Mwandishi Wetu, OMM TANGA**

MKOA wa Tanga unajulikana zaidi kwa kuwa ufukweni mwa bahari ya Hindi, lakini taarifa zinazohusu fursa zake nyingi bado hazijawafikia watu kwa kiwango kinachoweza kubadili kwa haraka fikra zao kuhusiana na mkoa huo.

Tanga ina fursa za uwekezaji ikiwamo rasilimali kama madini na misitu, ardhi, bahari, bandari, mali kale, fukwe nzuri na mbuga za wanyama kwa utalii ndani ya eneo lake la kilomita za mraba 2,764,534 lenye pwani na milima ya ndani kama Usambara. Kati ya hizo, hekta 1,893, 356 zinafaa kwa kilimo na hekta 686,556 bado hazijatumika.

Wakazi wengi hutegemea kilimo, ufugaji na uvuvi. Kati yao, zaidi ya asilimia 80 wamejikita katika kilimo, maliasili, utalii na wanaoishi maeneo ya mwambao wa bahari ya Hindi wanajishughulisha na uvuvi mdogo mdogo.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji Tanga, mkoa huo umeanisha maeneo makuu sita kwa ajili ya fursa za uwekezaji ambayo ni, uanzishaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na kilimo.

Mengine ni ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, kilimo cha biashara, bidhaa za maliasili, uwezeshaji na maeneo ya kutoa huduma kama vile hoteli, utalii, maduka, benki, masoko ya kisasa, maghala na wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo hayo.

Wakazi wengi hutegemea kilimo, ufugaji na uvuvi. Kati yao, zaidi ya asilimia 80 wamejikita katika kilimo, maliasili, utalii na wanaoishimaeneo ya mwambao wa bahari ya Hindi wanajishughulisha na uvuvi mdogo mdogo.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Fursa za Uwekezaji Tanga, mkoa huo umeanisha maeneo makuu sita kwa ajili ya fursa za uwekezaji ambayo ni, uanzishaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na kilimo.

Mengine ni ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, kilimo cha biashara, bidhaa za maliasili, uwezeshaji na maeneo ya kutoa huduma kama vile hoteli, utalii, maduka, benki, masoko ya kisasa, maghala na wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo hayo.

### Wilaya ya Tanga

Miongoni mwa fursa zilizopo ni maeneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali katika maeneo ya Gofu Chini, Pongwe, Amboni, Pingoni (Maweni) na Neema katika barabara ya Pangani. Kuna jumla ya viwanja 282 vyenye ukubwa wa wastani wa ekari kati 1.5 hadi 6.5 kwa kila kiwanja katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

*Inaendelea uk 40*

Inatoka uk 43

**Eneo la Viwanda la Kange**

Eneo hili lina ukubwa wa hekta 34.5 ambapo jumla ya viwanja 55 vinamilikiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Viwanja hivi vipo umbali wa kilomita saba kutoka Tanga mjini kwenye barabara ya Tanga – Segera, ambapo limemilikishwa kisheria kwa NDC.

**Eneo la Viwanda EPZA**

Eneo hili lina ukubwa wa hekta 1,300 ambalo lipo eneo la Neema, kandoni mwa barabara ya Tanga Pangani, na limepimwa ila bado halijaendelezwa.

**Wilaya ya Korogwe**

Korogwe pia ina fursa nyingi yakiwemo mazingira mazuri kwa ajili ya bandari kavu. Pia kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo, hekta 2,000 limeainishwa na kutengwa katika kata ya Mgombezi kwa ajili ya EPZ.

**Wilaya ya Handeni**

Handeni inafaa kwa uwekezaji katika sekta mbalimbali, Miongoni mwa hizo ni viwanda hasa vya uchakataji mazao ya kilimo. Kwenye kata ya Mkata (hekta 200), kijiji cha Msomera (hekta 150) na kata ya Segera (hekta 901).

Kata zilizopo pembezoni mwa barabara Segera-Chalinze ni maarufu kwa madini, kilimo cha machungwa na mananasi.

**Wilaya ya Muheza**

Ina fursa nyingi hasa katika viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na matunda. Miongoni mwa maeneo yaliyopo ni Songa, Kilulu, Mkuzi, Kwafungo na Makole.

Maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda pia yanapatikana katika kata za Bwebwera, Ngomeni na Kilulu na vijiji vya Misozwe na Kicheba ambako halmashauri imetenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Madini ya dhahabu yanapatikana Sakare, Kicheba, Amani na Mbambara na granite inapatikana Mkanyageni, Lihamba na chokaa inapatikana Pingoni.

**Wilaya ya Kilindi**

Kuna fursa za viwanda na katika maeneo ya Vyadigwa, Mbogo, Misufini na Kimamba. Pia kuna kilimo cha mboga hasa nyanya katika maneo ya Kikunde, Negero, Pagwi na Kilwa.

Maeneo mengine yanafaa kwa ufugaji ng'ombe wa maziwa, kilimo cha alizeti na imetenga maeneo ya Sangeni (hekta 833.30), Mkuyu (hekta 451.63), Mbwego (hekta 277.50 na Tobacco hekta 5,332.50.

Kilindi pia ina dhahabu maeneo ya Tunguli, Ngeze, Masagalu, Lwande, Mvungwe na Negero. Vito vya rubi na ganeti maeneo ya Kwamfyomi, madini ya kwatsi maeneo ya Chamtui, Kikunde, Kwediboma, Mbangwi, madini ya chaisedoni maeneo ya Negero na madini ya fildspa maeneo ya Negero na Kibirashi.

**Wilaya ya Lushoto**

Kuna fursa za ujenzi wa viwanda kwenye maeneo ya Mng'aro na Lunguza. Halmashauri ina hekta 2,500 za mashamba ya matunda katika maeneo ya kijiji cha Mnadani, kata ya Malindi na Lukozi.

Maeneo ya Ming'ao na Lunguza mwekezaji anaweza kujenga kiwanda cha kukoboa mpunga, kwani zao hilo linalimwa kwa wingi kwenye maeneo hayo.

Wilaya ya Lushoto pia imeanisha maeneo ya kijiji cha Mnadai, Lukosi na Malindi kwa ajili ya viwanda vya bidhaa za nyanya na Soni, Baga, Migwashi na Kwehangala kwa ajili ya kukusanya na kufungasha matunda na mazao mengine yanayolimwa wilayani humo.

Pia kuna fursa za viwanda vya chai na kahawa katika kata ya Gare (hekta 1,000). Kwemkazu ni maarufu kwa kilimo cha tangawizi ambako kuna mashamba ya hekta 460.

Lushoto kuna madini ya bauxite maeneo ya Manga, Mtindiro, Mabugha na Kwemasha, madini ya makaa ya mawe maeneo ya Lunguza na Maringo, shaba maeneo ya Mnazi, dhahabu maeneo ya Mponde na chumvi ya mawe maeneo ya Mombo.

**Wilaya ya Pangani**

Yametengwa maeneo maalumu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika kata ya Kipumbwi. Hekta 200 zimetengwa kwa ajili ya viwanda vya kuchakata mkonge maeneo ya Mkalamo, Masaika, Mkwaja, Mikungini na Mwera.

Katika eneo la Kilimangwido kuna mashamba ya mkonge hekta 4,400 za na Mizinga yana hekta 2,280 na kijijini Bushiri kuna hekta 400 za zao hilo.

Viwanda vya mafuta ya nazi vinaweza kujengwa Ubanga, Masaka na kata ya Pangani Magharibi. Wastani wa tani 16, 280 za nazi huzalishwa kila mwaka Pangani. Pangani pia kuna dhahabu maeneo ya Mlozo, chokaa maeneo ya Kimanga, chumvi maeneo ya pwani. Pia kuna fursa ya uwekezaji katika sekta ya samaki na ujenzi wa hoteli kwenye maeneo yote ya mwambao na maeneo ya kihistoria.



*Njia bora za usafirishaji ni miongoni mwa nyenzo zinazoashiria mazingira mazuri kwa uwekezaji eneo la Pongwe jijini Tanga.*

# UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA; KIPAUMBELE CHA MIPANGO MKOA WA TANGA



*Mfumo wa Mita 5 kwa 55 wa uhifadhi wa vyanzo vya Maji (Kushoto), na Kijito ambacho pembezoni mwake pamepandwa zao la Cacao katika Kijiji cha Shembekeza, Muheza – UWAMAKIZI*

**Na Mwandishi Wetu, OMM TAN-**

MAENDELEO endelevu ya Mkoa wa Tanga yanategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa rasilimali zilizopo kwenye mazingira.

Ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali hizo, uhifadhi na usimamizi wake vimekuwa suala la lazima katika kila ngazi mkoani humu, kuanzia mtu binafsi, kaya na taasisi za Serikali.

Taarifa ya Idara ya Uchumi na Uzalishaji ya Sekretarieti ya Mkoa huo inaeleza kuwa tanga ni miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na changamoto anuai za mazingira kama vile uharibifu wa ardhi, vyanzo vya maji, misitu, makazi ya wanyamapori, bayonuwai, mifumo ikolojia ya maji, uchafuzi wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, jitihada zinachukuliwa kukabiliana nazo ikiwemo kutunga sheria ndogo za halmashauri kuhusu usimamizi wa mazingira, kutenga fedha za kusimamia shughuli za mazingira, kuanzisha na kutekeleza programu za upandaji miti hususani kwenye vyanzo vya maji na kuanzisha Taasisi ya Hifadhi ya Bahari ya Kisukuku.

Nyingine ni kujenga dampo la kisasa kwenye kata ya Mpirani jijini Tanga, kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira, kuunda vikundi vya kijamii vya kuhifadhi mazingira, kuweka alama za kudumu kwenye vyanzo vya maji na misitu, na kufanya doria ya kudhibiti uvamizi na uharibifu.

Pia kuna mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini, utoaji vibali vya uvunaji wa miti, elimu ya ufugaji bora wa kisasa, elimu ya uzingatiaji wa sheria hususan kwa wakulima na wachoma mkaa.

Taarifa hiyo inazitaja jitihada nyingine ni utoaji elimu na uhamasishaji kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi na endelevu ya kilimo kinachohifadhi ardhi katika vijiji 20 vilivyopo maeneo ya milima ya Usambara Mashariki.

**Vyanzo vya maji**

Kwa mujibu wa taarifa ya Idara ya Uchumi na Uzalishaji, Tanga ina jumla ya vyanzo vya maji 810 vikiwemo visima virefu 117, mabwawa 38, maji mtiririko 95 na visima vifupi 560.

Zipo shughuli za kibinadamu zinazohatarisha uhai na uendelevu wake, hivyo hatua madhubuti zinachukuliwa kukabiliana na hali hiyo ikiwemo, kuanzisha na kusimamia kikundi cha Umoja wa Wakulima Wahifadhi Mazingira Kihukwi – Zigi (UWAMAKIZI), kinachohusika na uhifadhi wa mito wilayani Muheza.

Taarifa hiyo inazitaja hatua nyingine ni kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira na sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 katika ngazi za halmashauri, kwa kushirikiana na wadau wa mazingira.

***Inaendelea uk 46***

*Inatoka uk 45*

**Makazi ya wanyamapori, upotevu wa bayoanuai**

Hifadhi za wanyamapori ni miongoni mwa maeneo yanayoguswa na uharibifu wa mazingira. Tanga ina mbuga mbili za Saadan na Mkomazi zenye wanyamapori na pori tengefu la Umba lililopo wilaya za Lushoto, Korogwe na Mkinga.

Uharibifu wa makazi ya wanyamapori na upotevu wa bayonuai ni moja ya changamoto za kimazingira katika mkoa wa Tanga.

Baadhi ya sababu za uharibifu huo ni pamoja na jaamii ya wafugaji kuchunga mifugo kwenye hifadhi za wanyamakatika mbuga ya Mkomazi – Mwakijembe, na shughuli za uchimbaji wa madini zinazofanyika katika maeneo ya Mwakijembe katika kijiji cha Mkota wilayani Mkinga.

Hali hiyo imepelekea baadhi ya athari ikiwemo migogoro kati ya binadamu na wanyamapori ambapo, wananchi huvamiwa na wanyama ikiwemo tembo wanaofika mara kadhaa kwenye makazi ya watu.

Ili kuidhibiti hali hiyo, hatua kadhaa zinachukuliwa ikiwa ni pamoja na kushirikiana na TAWA kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na kupambana na tembo ikiwemo kutumia pilipili.

**Uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya maji**

Mifumo ya ikolojia ya maji kwenye mkoa wa Tanga, inajumuisha mazingira na maisha na viumbehai wanaopatikana kwenye maeneo ya bahari, ikihusisha Matumbawe, Mikoko, Samaki, Nyasi Bahari na rasilimali zinginezo.

Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na uharibifu wa mifumo ya ikolojia ni pamoja na kuanzishwa Taasisi ya Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga, (TCMP) jijini Tanga, maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi na kusini mwa kijiji cha wavuvi cha Kigombe wilayani Muheza, kwa ajili ya kulinda mifumo ikolojia na rasilimali za bahari hususan samaki aina ya Silikant.

**Upandaji miti**

Mkoa umeendelea na mkakati wa kutekeleza agizo la kitaifa la upandaji miti kwa kila halmashauri kupanda miti 1,500,000. Hivyo jumla ya miti 11,493,616 imepandwa, ikiwa ni sawa na asilimia 84.8 ya malengo ya kupanda miti 16,500,000.



*Matumbawe na Samaki aina ya Silikanti katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti, Tanga*

# UCHUMI WA BULUU 'UNAVYOPAA' KUIINUA TANGA

**Na Mwandishi Wetu, OMM TANGA**

UWEPO wa bahari ya Hindi kwenye eneo la Mkoa wa Tanga, unalifanya eneo hilo kuwa mionhgoni mwa maeneo yanayoguswa na uchumi wa buluu, hivyo kuwa wanufaika wa rasilimali za baharini.

Uchumi wa buluu katika Tanga unajumuisha ufugaji wa viumbe-bahari, uvuvi, utalii wa baharini na juhudi za uhifadhi, zote zikiwa na lengo la kuboresha maisha na kuongeza uchumi wa mkoa huo na taifa kwa ujumla.

**Ukuzaji viumbe-bahari**



Taarifa ya Idara ya Uchumi na Uzalishaji ya Sekretarieti ya Mkoa (RS) inaeleza kuwa, Tanga inashuhudia mageuzi makubwa katika ukuzaji wa viumbe- bahari kama shughuli muhimu katika uchumi wa buluu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, idadi ya wakulima wa mwani imeongezeka kutoka chini ya 500 mwaka 2021 hadi 5,300, huku uzalishaji ukifikia tani 3,000 kwa mwaka, na kuingiza zaidi ya Shilingi bilioni 6.

Aidha, kufufuliwa kwa Kituo

*Inaendelea uk 47*

*Inatoka uk 46*

cha Machui Marine Hatchery kunalenga kuzalisha vifaranga vya kaa na majongoo bahari, kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao haya kwa soko la ndani na nje ya nchi.

Taarifa inaeleza, fursa katika ukuzaji viumbe- bahari ni kubwa sana ikichagizwa na bahari inayohimili shughuli hizo kwa ukubwa wake, utayari wa wananchi katika maeneo ya bahari, utashi wa Serikali ya Mkoa na Mamlaka za Serikaliza Mitaa na uwepo wa taasisi mbalimbali za serikali na za binafsi zinazojihusisha na ukuzaji viumbe- bahari katika mkoa.

**Uvuvi**



Taarifa hiyo inaeleza, Tanga ina zaidi ya wavuvi 13,000 na inaendelea kuboresha uvuvi wa samaki kupitia matumizi ya teknolojia bora, na utekelezaji wa mbinu endelevu za uvuvi.

Uwekezaji katika maeneo ya mialo ya samaki, hifadhi za baridi, na uvuvi wa maji marefu bado una fursa kubwa mkoani humo na utarahisisha upatikanaji wa mazao ya uvuvi na kupunguza upotevu wa mazao ya baharini baada ya kuvuliwa.

Sekta ya uvuvi inabaki kuwa chanzo kikuu cha ajira na kipato kwa jamii za pwani na Mamlaka zake za Serikali za Mitaa.

**Uhifadhi wa Bahari**

Juhudi za kuhifadhi bioanuwai ya baharini zinajumuisha ulinzi wa misitu ya mikoko na nyasi-bahari, urejeshwaji wa miamba ya matumbawe, ulinzi wa viumbe vilivyo kwenye hatari ya kupotea na matumizi ya mbinu rafiki za uvuvi.

Mkoa wa Tanga unashirikiana na wadau mbalimbali kama vile Wildlife Conservation Society (WCS), Mwambao Coastal Community Network, International Union for Conservation of Nature (IUCN), na Seasense, kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, ukiongozwa na kaulimbiu ya Bahari Yetu, Maisha Yetu!

Kaulimbiu hii inawachochea wananchi kutambua kuwa, kutoitunza bahari ni kuharibu maisha yao ya sasa na ya vizazi vijavyo.

Aidha, uwepo wa Tanga Coelacanth Marine Park (TACMP) katika bahari yetu, kunahakikisha ulinzi thabiti wa rasilimali za bahari na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika uchumi wa buluu.

**Utalii wa Baharini**

Fukwe za kuvutia za Tanga, ikiwemo Pangani na hifadhi ya taifa ya Saadani, visiwa saba vilivyopo chini ya TACMP katika wilaya za Tanga na Mkinga, zinatengeneza kivutio vikuu vya utalii wa baharini na fursa adhimu kwa sekta ya utalii- bahari.

Uendelezaji wa mifumo endelevu ya utalii na uhifadhi endelevu unahamasisha uwekezaji katika sekta ya utalii kupitia mahoteli, michezo ya majini, na utalii wa kiikolojia, hivyo kuleta wigo mpana wa shughuli za kiuchumi katika mkoa huu.



# BILIONI 4.513 ZILIVYOLETA KITUO BORA CHA MICHEZO TANGA



*Vijana wakiwa kwenye mazoezi ya mpira wa miguu katika Kituo cha Ufundi cha Michezo mkoani Tanga kinachomilikiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF)*

**Na Mwandishi Wetu, OMM TANGA**

SEKTA ya michezo ni sehemu ya maeneo muhimu yanayopiga maendeleo kwa kasi, kupitia utendaji kazi ya Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan.

YMkoa wa Tanga umekuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa katika sekta hiyo, ambapo pamoja na jitihada za Serikali, wadau hasa waliopo kwenye sekta binafsi.

Yapo mambo mengi yaliyofanyika mkoani Tanga katika kukuza sekta ya michezo, miongoni mwa hayo ni ujenzi wa kituo bora za kukuza vipaji hasa kwa vijana na watoto.

Tanga ilipokea Shilingi bilioni 4.513 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Ufundi cha Shirikisho la Michezo Tanzania (TFF) katika eneo la Mnyanjani jijini Tanga.

Miundombinu iliyojengwa katika eneo hili ni pamoja na viwanja viwili vikubwa vya mpira wa miguu ambapo kimoja kati ya hivyo, kimetengenezwa kwa nyasi bandia na kingine kikiwa na nyasi za asili.

Pia mradi huo ukahusisha ujenzi wa majengo ya utawala, hosteli, madarasa. Miundombinu hiyo inatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama malazi na mafunzo mbalimbali kwa walimu wa mpira wa miguu, wanamichezo hususani vijana na watoto.

Lengo ni kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanamichezo hao.



*Wallece Karia - Rais wa TFF*

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe Balozi Dkt. Batilda Burian (wa nne kushoto) akishiriki utoaji mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ya jiji la Tanga hivi karibuni.*



*Mbunge wa Pangani ambaye pia ni Waziri wa Maji, Mhe Jumaa Aweso (wa pili kulia) akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Pangani, Bw. Charles Edward Fussi boksi la madaftari yaliyokuwa sehemu ya vifaa vya elimu kwa wanafunzi jimboni humo.*



*Naibu Waziri Mkuu, Dk Doto Biteko (kulia) akipiga makofi baada ya kufungua Shule ya Sekondari Miles and Kimberly White iliyopo Mkinga mkoani Tanga.*



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe Balozi Dkt. Batilda Burian (aliyeketi nyuma kushoto) akiwa na Mstahili Meya wa Jiji la Tanga, Mhe Abdurahaman Shiloow (kulia kwake) kwenye moja ya bajaji zilizotolewa kupitia mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.*



*Miongoni mwa magari yaliyotolewa na Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwa Wakuu wa Wilaya na Mkuu wa Idara ya Mipango mkoani Tanga.*



*Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Mhe Gift Msuya akikagua miundombinu ya maji kabla ya kuzinduliwa wilayani humo.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe Balozi Dk Batilda Burian (kulia) akiwa katika moja ya ziara zake za kusikiliza kero za wananchi.*



*Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mh Balozi Dk Batilda Burian (kulia) akimpokea Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe Jerry Silaa alipomtembelea ofisini wake hivi karibuni.*



*Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (kushoto) akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa huo, Mhe Balozi Dk Batilda Burian kuhusu magari yaliyotolewa na Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwa Wakuu wa Wilaya na Mkuu wa Idara ya Mipango wa Sekretarieti ya Mkoa huo.*



*Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Mh William Mwakilima (aliyenyoosha mkono) akiwa katika moja ya ziara zake za kikazi wilayani humo. Aliyevaa kofia katikati ni Katibu Tawala Wilaya hiyo, Mwanaidi Adadi.*



*Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdulraham Abdallah (kushoto) akiwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT), Mary Chatanda kwenye msiba wa aliyekuwa Katibu wa Mkoa wa CCM, marehemu Seleman Sankwa.*



*Afisa Habari Msaidizi wa Mkoa wa Tanga, Emma Kigombe (kushoto) akiwa na cheti cha tuzo ya umahiri mahali pa kazi iliyotunukiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Kitengo cha Mawasiliano cha Sekretarieti ya Mkoa huo hivi karibuni. Kulia ni Katibu Tawala Mkoa, Pili Mnyema.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mhe Japhari Kubecha (kushoto) akikabidhi mmoja wa Maafisa Ugani pikipiki zilizotolewa na Mhe Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwa wataalamu hao.*



*Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mh Japhari Kubecha (nyuma) akisafiri kwa kutumia moja ya pikipiki zilizotolewa kwa Maafisa Ugani wilayani humo.*



*Mradi wa maji kwenye kata ya Mkwaja, wilaya ya Pangani mkoani Tanga, uliozinduliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhe Gift Msuya (hayupo pichani).*




*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe Balozi Dk Batilda Burian (wa tano kushoto) alipozindua kambi ya macho wilayani Muheza na kugawa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi milioni 400 vilivyotolewa na Mhe Rais Dr Samia Suluhu Hassan.*



*Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mh Ashatu Kijaji (kushoto) akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiomoni ya jijini Tanga. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mh Balozi Dk Batilda Burian.*



*Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mh Albert Msando (kulia) akikabidhi jiko linalotumia gesi kwa Sheikh wa Wilaya ya Handeni, Alhaji Shabani Kizulwa*

**Jarida hili limeandaliwa na:**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga,
S.L.P 5095,
**TANGA.**
ras.tanga@tamisemi.go.tz
www.tanga.go.tz
@rc_tanga_official
tanga mkoa tv

**TIMU YA UHARIRI**
**Mhariri Mkuu**
•Mashaka Bonifas Mgeta - 0754691540
RS Tanga
**Mpiga Picha Mkuu**
•Emma Kigombe - 0679952981
RS Tanga

**WAANDISHI WA HABARI**
•Laban Mussa – 0715179070
Tanga Jiji
•Martine Kamote, - 0719 240 528
Pangani
•Nassoro Rashid - 0713 829207
Mkinga
•Ester Mbusi - 0689551111
TSB Tanga
•Cyprian Luanda - 0718102260
Handeni DC
•Job Karongo - 0787404 165
Handeni TC
•Siwema Salum - 0654214796
Muheza
•Seleman Shineni - 0714 175 740
•Lushoto
•Jumanne Semagongo – 0713867353
Korogwe TC
•Omari Mwinjuma - 0714944048
Korogwe DC
•Vumilia Ngajua – 0695 596650
Bumbuli